# Nipashe

Jumanne Oktoba 24, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581473

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



UK. 22

**MOURINHO AISHANGAA KADI YAKE NYEKUNDU**



# Tundu Lissu aibua hoja mikataba ya Bandari

UKURASA 3

UKURASA WA 4

## MABASI 19 YAPIGWA KUFULI KUTOA HUDUMA

MABASI 19 yanayotoa huduma ya usafirishaji mkoani Geita, yamefungiwa kutoa huduma hiyo kutokana na kuwa mabovu na...

UKURASA WA 10

## WAKULIMA WASUSA KILIMO CHA MPUNGA



WAKULIMA wa mpunga wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, wameachana na kilimo hicho kutokana na ukame...

## Mtanzania aeleza 'kutoweka' mwanawe Israel kwa siku 18

UKURASA 5





Rais Samia Suluhu Hassan akipokea picha ya Majaji Wakuu wa Nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika kutoka kwa Mwenyekiti wa Jukwaa lao, ambaye ni Jaji Mkuu wa Namibia, Peter Shivute, katika mkutano uliofanyika jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Samia awapa angalizo majaji wakuu utatuzi wa migogoro

UKURASA 2

UKURASA WA 7

**SMZ** yajenga hospitali wilaya, yabinafsisha uendeshaji wake

UKURASA WA 7

**Benki** zajipanga kukabiliana na tishio la El-Nino



UKURASA WA 8

**CCM** yasimamisha viongozi kashfa ya kuhujumu chama

**MICHEZO** **YANGA SC, AZIZ KI WAKAA KILELENI** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Samia awapa angalizo majaji wakuu utatuzi wa migogoro

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amezitaka mahakama za kitaifa na majaji wakuu wa nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika (SEACJF), kujipanga kufanya usuluhishi wa migogoro inapotokea kwenye eneo huru la biashara la Afrika (AfCFTA), na kusisitiza kuwa hilo ni eneo kubwa zaidi la biashara huria duniani.

Akizungumza jana jijini hapa, wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka wa jukwaa la majaji wakuu wa nchi hizo, Rais Samia aliwataka majaji hao kwenda kuzijengea uwezo mahakama katika nchi hizo ili ziwe na uwezo wa kutatua migogoro hiyo.

"Ni ukweli uliothibitishwa kwamba eneo la biashara huru la Bara la Afrika, si ndoto tena, bali ni ukweli. Eneo la biashara huru la Bara la Afrika, liliteuliwa kuwa mojawapo ya programu kuu za ajenda 2063. Afrika tunayoitaka mafanikio yake hayawezi kufikiwa ipasavyo bila utambuzi unaostahili wa mahali na jukumu la kuwezesha la mahakama zetu za kitaifa katika kutatua mizozo ya biashara ya ndani na ya mipakani," alisema.

Mkutano huo wa siku tano ulionza jana, unaendelea hadi Oktoba 27, mwaka huu, ukitanguliwa na kaulimbiu: 'Wajibu wa mahakama za kitaifa katika utatuzi wa migogoro kwenye eneo huru la biashara Afrika; matumizi ya teknolojia ya kisasa ili kuongeza ufanisi katika teknolojia'.

Utatuzi wa migogoro hiyo kwenye eneo huru la biashara la Afrika, utasaidia kuondoa vizuizi vya kuingia na kupanua matarajio ya sekta binafsi, kufikia soko la Afrika kwa upana zaidi.

Aidha, Rais Samia akizungumza katika jukwaa hilo, alisema ukuaji wa soko katika Eneo Huru la Biashara barani Afrika, utazalisha changamoto kadhaa ambazo lazima mahakama ziweze kusimama na kuzitatua.

Vilevile, Rais Samia alisema, ukuaji wa teknolojia na ubunifu ni moja kati ya mambo yanayoweza kusababisha migogoro na miingiliano na kwamba mahakama ni lazima zijipange kusuluhisha migogoro ya aina hiyo inapotokea.



Alizitaka mahakama za kitaifa kuona umuhimu wa kutumia teknolojia za kisasa katika kusikiliza na kutatua migogoro mbalimbali ya kibiashara inayojitokeza katika eneo hilo.

Kuhusu mafanikio ya matumizi ya teknolojia katika Mahakama ya Tanzania, Rais Samia, aliipongeza akieleza namna alivyoliona janga la UVIKO-19, lilivyoacha funzo muhimu kwa mataifa na taasisi mbalimbali, na kwamba mahakama hiyo haikuacha kuendelea na majukumu yake.

"Kwa hapa Tanzania tuliweka shutdown (funga), lakini hatukuweza kuacha kufanya kazi. Tulitumia teknolojia za kisasa katika kutoa huduma kwa wananchi katika sekta mbalimbali, mahakama ikiwa mojawapo.

"Mojawapo ya maeneo ambayo tuliangazia na kusambaza suluhisho lililokubaliwa la kupunguza athari mbaya za COVID-19 lilikuwa ni usimamizi wa haki au watu kupitia msaada wa suluhisho la teknolojia ya nyumbani.

...Mahakama yetu haikuweza tu kudumisha upatikanaji wa haki kwa wote ninaowahitaji, bali pia iliweza kujihakikishia usalama yenyewe."

Awali, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, katika hotuba yake, alisema Jukwaa la Majaji Wakuu wa Nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika, kila mwaka wakikutana hujadili masuala yanayowakabili wananchi wa Afrika na kuyatafutia ufumbuzi.

Kwa mujibu wa Jaji Mkuu, mwaka huu, mjadala mrefu wa jukwaa hilo utahusu eneo huru la biashara Afrika.

Prof. Juma alisema, mjadala wa namna hiyo unawasaidia majaji wakuu kuwa na maamuzi ya pamoja kuhusu mambo mbalimbali yanayowakabili wananchi wa Afrika na kuwa na kauli ya pamoja kukabiliana nayo.

Alisema maazimio yanayotolewa katika jukwaa hilo yamekuwa na manufaa kwenye kufanya uamuzi na kuwezesha mhimili wa mahakama kuwa karibu na jamii wakati wote.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
24.10.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 26-10-2023 hadi 29-10-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero kupitia Mikumi,** gari hiyo ina namba ya usajili: **T 453 DYG / T 881 EAU**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 20.00** |
| **Upana** | - | **mita 5.10** |
| **Kimo** | - | **mita 5.50** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


## Kamati ya Bunge yapewa taarifa ya mikakati kuzuia uchafuzi mazingira

**Na Robert Hokororo,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, amesema serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, imeibua miradi ya kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia taka nchini.

Aliyasema jana alipowasilisha taarifa ya utekelezaji mikakati ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira kwenye mito na mifereji katika Jiji la Dar es Salaam, mafanikio na changamoto kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira jijini Dodoma.

Khamis alisema serikali ilitoa mwongozo wa usafishaji mito kwa lengo la kuondoa taka ngumu, mchanga na tope kwa mito ya Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza madhara yanayoweza kutokea kutokana na uchimbaji holela wa mchanga katika mito hiyo.

Alisema katika utekelezaji mwongozo, usafishaji ulianza katika mito mitano na hadi sasa jumla ya mito tisa mkoani humo; Msimbazi, Mbezi, Tegeta, Nyakasangwa, Mpiji Luhanga, Kibangu, Kibwegere na Kigori imeanza kusafishwa.

Naibu Waziri Khamis alitaja mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na uchafuzi wa mito na mifereji kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa usafi wa mito katika maeneo ya jiji. Jumla ya urefu wa eneo la mito lililosafishwa ni mita 99,677. Makandarasi wamesafisha mita 41,150 na vikundi vya machepe mita 58,527.

Pia alisema uimarishaji kingo za mito umefanywa. Miti rafiki kwa mazingira 24,000 imepandwa katika maeneo mbalimbali kama vile Mto Msimbazi eneo la Pugu Station, Mto Mpiji maeneo ya Mgemuzi, Mabwepande Mitiki na Mbweni.

Dar es Salaam ni mojawapo ya majiji makubwa likiwa na jumla ya watu milioni tano kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, ongezeko likiambatana na shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa changamoto za kimazingira ikiwamo uchafuzi unaotokana na taka ngumu na taka maji.

Kulingana na takwimu za hivi karibuni, uzalishaji wa taka ngumu ni wa wastani wa tani 4,161 kwa siku ambapo kati ya hizo, uwezo wa halmashauri kukusanya taka ni asilimia kati ya 45 hadi 50 tu.

Hivyo, zaidi ya asilimia 50 ya taka hubaki kwenye mazingira na kuzagaa hadi kwenye mito na mifereji ya majitaka na mitaro ya maji ya mvua.

Changamoto hii huchangia kuziba kwa mifereji, mitaro na mito na hivyo kusababisha mafuriko nyakati za mvua.


**TAARIFA KWA UMMA**

TADB
Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania



Asha Hussein Tarimo

**Tunapenda kuutaarifu umma kuwa Asha Hussein Tarimo pichani sio mtumishi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kuanzia tarehe 23 Oktoba 2023.**

**Hivyo TADB haitahusika wala kutambua kwa namna yoyote ile mikataba, mawasiliano au shuhuli zozote zitakazofanywa na mtajwa ambae picha yake inaoneka kushoto kuanzia tarehe 23 Oktoba 2023.**

**IMETOLEWA NA: UONGOZI WA TADB**

# Tundu Lissu aibuka mikataba Bandari

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema kuna haja mikataba ya uwekezaji na uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kuwekwa wazi kwa Watanzania ili kila mwananchi aisome.

Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, ametoa kauli hiyo ikiwa ni siku moja baada ya Serikali ya Tanzania na Mamlaka ya Dubai kupitia Kampuni ya DP World kutia saini mikataba mitatu ya uwekezaji na uendeshaji bandari hiyo.

Mwanasiasa huyo alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Columbus, Ohio nchini Marekani.

Alisema kwa kuwa serikali imeeleza kwamba ilizingatia maoni ya Watanzania yaliyotolewa awali kuyaweka katika mkataba huo, ni vyema mkataba ukawekwa hadharani ili kila mwananchi ausome.

"Serikali imetuambia kwamba maoni ya wananchi katika mkataba huo yamezingatiwa. Kwa hiyo, hayo maneno mazuri ambayo tumeambiwa kwamba mawazo yamezingatiwa ni vyema yakawekwa wazi kuonesha mikataba yenyewe kwa uthibitisho zaidi ili kila mwananchi aone na asome kila kitu kilichomo katika mikataba kwa uwazi zaidi.

"Na ninasema ni vyema kufanya hivyo kwa sababu hili jambo lina uzito mkubwa na lilivuta hisia za wengi. Kwa hiyo, ili kuleta imani kwa wengi waliokuwa na wasiwasi tangu awali, ni vyema (mikataba) ikawekwa wazi.

"Nilikuwa ninafuatilia ile hafla wakati mikataba hiyo inatiwa saini, lakini sikuona hata nakala moja ambayo ilitolewa kwa watu ili wasome. Tunataka waiweke wazi na sisi tusome. Kuna msemo unasema 'seeing is believing' (kuamini ni kuona), tunataka tuone!" Lissu alisisitiza.

Katika hafla ya utiaji saini mikataba hiyo iliyofanyika juzi Ikulu mkoani Dodoma, mikataba iliyotiwa saini ni wa nchi mwenyeji, wa upangishaji ardhi na wa uendeshaji gati namba nne hadi saba katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mikataba hiyo ilitiwa saini kutokana na kukamilika mazungumzo ya pande hizo mbili pamoja na kutiwa saini kwa makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Mamlaka ya Dubai kuhusu uwekezaji (IGA) Oktoba 24 mwaka jana.

Hata hivyo, makubaliano ya pande hizo mbili yalikosolewa na wadau mbalimbali, hata baadhi ya wakosoaji kutishia kuitisha maandamano nchi nzima, lakini Serikali ya Tanzania ikasisitiza mkataba huo utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi.

Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini juzi, alisema maslahi ya nchi katika mikataba hiyo yamezingatiwa na hakuna sauti iliyopuuzwa, huku akisisitiza kwamba sheria za Tanzania zitatumika katika utekelezaji mikataba hiyo.

Kwa mujibu wa Zuhura Yunus, Mkurugenzi wa Mawasiliano Ofisi ya Rais, Ikulu, mikataba hiyo mitatu imetiwa saini kwa kuzingatia kifungu cha 2 cha Sheria ya Ubia Na. 6 ya Mwaka 2023 na Kifungu cha 2 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 5 ya Mwaka 2023.



# CHAKUHAWATA yaendelea kuchota wanachama wa CWT

**Na Steven William,**
MUHEZA

CHAMA cha Kulinda na Kutetea Haki za Walimu Tanzania (CHAKUHAWATA) wilayani Muheza, Tanga kimepata viongozi wapya, huku kikichukua wanachama 320 waliotoka Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

Uchaguzi huo umefanyika wilayani Muheza, mgeni rasmi akiwa Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Cyprian Mselem.

Katika uchaguzi huo wanachama wa chama hicho waligombea uongozi katika ngazi mbalimbali na kunadi sera zao kwa wajumbe waliohudhuria.

Akisoma matokeo ya uchaguzi huo mwakilishi wa Katibu Mkuu wa chama, Goodhope Michael, alisema uchaguzi nafasi ya Mwenyekiti wa Wilaya imechukuliwa na Seraphin Mvungi.

Alisema nafasi ya katibu imechukuliwa na Tumaini Peter, nafasi ya mwekahazina imekwenda kwa Habibu Shedafa na nafasi ya mwakilishi wa walimu imechukuliwa na Allan Kiondo.

Wengine waliochaguliwa katika uongozi huo ni mwakilishi walimu wa kike, Asha Kitambazi, nafasi ya mwakilishi walimu wenye ulemavu, Mariam Hamad na nafasi ya mwakilishi taasisi za elimu, Festo Mnkeni.

Baada ya kutangaza matokeo hayo, aliwaomba wanachama na viongozi wafanye kazi kwa ushirikiano, kusiwe na makundi ndani ya chama.

Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi huo, Anna Elius, alisema kuwa hivi sasa wamepata uongozi na wamejipanga kuhakikisha wanazunguka wilaya nzima ya Muheza kuzungumza na walimu ili waingie katika chama hicho.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Mselem alisema halmashauri hiyo inafanya kazi kwa kushirikiana na chama hicho, huku akiwataka viongozi waliochaguliwa kuwa waadilifu ndani ya chama. Waepuke migogoro.

## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED
## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

1st Housing

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2023**
(Kiasi kwa shilingi elfu)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30th Sept. 2023 | Robo Mwaka iliyopita 30th Jun. 2023 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 524 | 79 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,656,281 | 3,598,778 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,754,195 | 4,881,113 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 24,063,119 | 22,841,491 |
| 12 | Mali Nyingine | 942,817 | 901,852 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 251,211 | 275,507 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **35,290,147** | **34,120,820** |
| | | | |
| B. | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 1,533,034 | 1,247,409 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 555,922 | 571,677 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 414,347 | 384,598 |
| 27 | Dhima Nyingine | 283,389 | 389,517 |
| 28 | Madeni | 13,795,332 | 12,920,370 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **16,582,024** | **15,513,570** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **18,708,123** | **18,607,251** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,581,398) | (3,559,082) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 206,918 | 106,045 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 186,773 | 164,457 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **38** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,708,123** | **18,607,251** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 912,950 | 960,319 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 285,616 | 207,933 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 53.01% | 54.53% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.75% | 4.16% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 1477.27% | 1657.39% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 68.19% | 66.94% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89.51% | 86.26% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 22.90% | 9.96% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 3.43% | 3.92% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2023** (Kiasi kwa shilingi elfu)

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa 30th Sept. 2023 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30th Sept. 2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30th Sept. 2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30th Sept. 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,196,583 | 1,021,946 | 3,348,350 | 2,589,359 |
| 2 | Gharama za Riba | (370,266) | (334,602) | (1,027,741) | (663,909) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **826,317** | **687,344** | **2,320,609** | **1,925,449** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (77,683) | (13,584) | (133,256) | (48,786) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **119,451** | **67,954** | **292,439** | **258,495** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,238 | 47 | 1,345 | 136 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 79,206 | 59,347 | 244,938 | 166,736 |
| | 6.3 Gawio | 36,900 | - | 36,900 | 27,590 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 2,106 | 8,559 | 9,256 | 64,032 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(760,817)** | **(709,776)** | **(2,254,855)** | **(2,019,806)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (398,565) | (362,484) | (1,189,972) | (1,021,911) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (362,252) | (347,292) | (1,064,883) | (997,895) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **107,268** | **31,938** | **224,937** | **115,352** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (6,396) | (5,299) | (18,019) | (13,951) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **100,872** | **26,638** | **206,918** | **101,401** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **100,872** | **26,638** | **206,918** | **101,401** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 25 | 23 | 25 | 23 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.46 | 0.12 | 0.95 | 0.47 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.29% | 0.08% | 0.29% | 0.08% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.54% | 0.15% | 0.54% | 0.15% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 80.44% | 93.97% | 86.29% | 92.48% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.71% | 2.30% | 2.71% | 2.30% |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2023** (Kiasi kwa shilingi elfu)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30th Sept. 2023 | Robo ya Mwaka iliyopita 30th Jun. 2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30th Sept. 2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30th Sept. 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **107,268** | **61,581** | **224,937** | **115,352** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 97,714 | (417,296) | (319,582) | 246,195 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,288,970) | (1,512,294) | (4,733,165) | (5,199,520) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 285,625 | 113,005 | 621,247 | 253,602 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (110,152) | 29,405 | 139,927 | 398,104 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (22,945) | (68,394) | (218,045) | (161,817) |
| | - Kodi iliyolipwa | (18,019) | (11,624) | (18,019) | (13,951) |
| | - Mengineyo | 22,363 | 50,443 | 61,182 | 76,752 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(927,118)*** | ***(1,755,173)*** | ***(4,241,518)*** | ***(4,285,285)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (6,076) | 603,409 | 623,797 | (32,598) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (57,502) | 57,202 | (54,918) | (51,482) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(63,578)*** | ***660,611*** | ***568,879*** | ***(84,080)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu kwenda CRDB | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Deni jipya kutoka CRDB Bank | 874,962 | 1,033,901 | 1,791,603 | 10,991,291 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | (50,445) | (73,531) |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***874,962*** | ***1,033,901*** | ***1,741,158*** | ***10,917,760*** |
| | | | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha** | **(115,734)** | **(60,661)** | **(1,931,481)** | **6,548,396** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 4,881,192 | 4,942,251 | 6,696,939 | 945,786 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | (10,739) | (398) | (10,739) | (3,221) |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **4,754,719** | **4,881,192** | **4,754,719** | **7,490,961** |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2023** (Kiasi kwa shilingi elfu)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (30.09.2023)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.07.2023)** | **21,800,000** | **-** | **(3,453,037)** | **164,457** | **-** | **95,831** | **18,607,251** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 100,872 | - | - | - | 100,872 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (22,316) | 22,316 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (30.09.2023)** | **21,800,000** | **-** | **(3,374,481)** | **186,773** | **-** | **95,831** | **18,708,123** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (30.06.2023)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.04.2023)** | **21,800,000** | **-** | **(3,440,699)** | **96,483** | **-** | **95,831** | **18,551,615** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 55,636 | - | - | - | **55,636** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | **(67,974)** | **67,974** | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (30.06.2023)** | **21,800,000** | **-** | **(3,453,037)** | **164,457** | **-** | **95,831** | **18,607,251** |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

**MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES FOR THE YEAR 2023**

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 16% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Restructuring/Rescheduling Fee | 1% of the restructured/ rescheduling amount |
| 7 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 8 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 9 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid |
| 10 | Annual Review Fee | NIL |
| 11 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 12 | Loan Statement | TZS 20,000/- |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| *Jina na Cheo :* | *Saini* | | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | (Imesainiwa) | .............................. | **25.10.2023** |
| Amulike E. Kamwela **(Mkuu wa Fedha)** | (Imesainiwa) | .............................. | **25.10.2023** |
| Isambo Binde **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | (Imesainiwa) | .............................. | **25.10.2023** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| *Jina:* | *Saini* | | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| Conrad D'souza **Mwenyekiti** | (Imesainiwa) | .............................. | **25.10.2023** |
| Margaret Ikongo **Mkurugenzi** | (Imesainiwa) | .............................. | **25.10.2023** |



2176663602

# Mabasi 19 yapigwa kufuli kutoa huduma usafirishaji

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MABASI 19 yanayotoa huduma ya usafirishaji mkoani Geita, yamefungiwa kutoa huduma hiyo kutokana na kuwa mabovu na kutokukidhi vigezo vya kutoa huduma hiyo kwa mujibu wa sheria.

Mabasi hayo ni kati ya magari 214 yaliyofanyiwa ukaguzi na Jeshi la Polisi mkoani Geita kupitia Kitengo cha Usalama Barabarani kilichobaini makosa mbalimbali katika mabasi 142 huku 19 yakikoswa vigezo vya kuendelea na kazi hiyo.

Akitoa taarifa ya operesheni hiyo iliyofanyika kuanzia Oktoba 19 mwaka huu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi Safia Jongo, alisema kuwa kati ya mabasi hayo 214, mabasi 53 pekee hayakukutwa na makosa, hivyo kuruhusiwa kuendelea na shughuli zao za usafirishaji.

Alisema ukaguzi huo ulijumuisha mabasi yote makubwa na madogo yanayofanya shughuli za usafirishaji ndani ya mkoa huo uliofanyika katika Stendi Kuu ya Mabasi Geta.

Kamanda huyo alisema huyo magari hayo yaliyofungiwa hayakukidhi vigezo vya kubeba abiria kutokana na kuwa mabovu, hivyo yamepigwa marufuku kujihusisha na biashara ya kubeba abiria.

Magari hayo ni pamoja na yanayofanya safari za kutoka Geita kwenda jijini Mwanza, Shinyanga, Geita na mengine yanayofanya safari ndani ya mkoa huo yakitoka mjini Geita kwenda maeneo ya Katoro, Nkome, Nyarugusu na Nyang'hwale.

"Magari 142 yamekutwa na makosa mbalimbali ikiwamo kutokuwa na mikanda ya kuvaa abiria pamoja na makosa mengine. Wamiliki wake wamepigwa faini na kuendelea na safari. 53 yamekaguliwa na hayakukutwa na makosa," alisema.

Kamanda huyo alisema lengo la operesheni hiyo ni kudhibiti matukio ya ajali za barabarani ambazo zimekuwa zinajitokeza hususani katika kipindi cha msimu wa sikukuu pale wasafiri wanapoongezeka kwa kiwango kikubwa.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Geita, Mrakibu wa Polisi Aloys Jacob, alisema kuwa kwa kuzingatia sheria, madereva wa magari hayo watafikishwa mahakamani kwa mujibu wa kifungu namba 36 cha Sheria ya Makosa ya Usalama Barabarani.

"Wamiliki wa magari makubwa na magodo pamoja na madereva waliojidanganya kuficha magari watambue kuwa operesheni hii ni endelevu, hivyo hakuna gari litakalobaki bila kukaguliwa," alisema.

Wiki iliyopita, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani liliiambia Nipashe kuwa katika miezi tisa iliyopita, kulitokea ajali za barabarani 1,334 zilizosababisha vifo vya watu 1,198, sawa na wastani wa vifo vya watu 133 kila mwezi nchini.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vivo Energy Tanzania, Mohamed Bougriba (wa tatu kulia) na Ofisa Elimu wa Manispaa ya Temeke, Abdul Buhety (wa pili kulia), wakikata utepe katika hafla ya kukabidhi choo chenye matundu 16 kilichokarabatiwa na kampuni hiyo kwa Shule ya Msingi Kiungani iliyopo Kurasini Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Bonivilia Malya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali kunufaika mikopo ya kilimo

**Na Halfani Chusi**

KATIKA kuwainua wakulima, Taasisi ya Victoria Finance kwa kushirikiana na PASS Trust, wametangaza kutoa mikopo kwa wajasiriamali wa kilimo kupitia dhamana ya mikopo kwa njia ya kidijitali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Victoria Finance, Julius Mcharo, aliwaambia waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana kuwa lengo lao ni kutoa mitaji kwa wajasiriamali wa kilimo nchi nzima.

Alisema wameanzisha huduma hiyo ya mikopo kidijitali ili kukidhi mahitaji ya mitaji kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo walio katika mnyororo wa thamani wa kilimo, ikiwa ni pamoja na wale wanaojihusisha na biashara za mazao ya kilimo na mifugo.

Mcharo alisema kuwa kwa kutambua changamoto wanazokabiliana nazo wajasiriamali, taasisi hiyo imeanzisha aina mbalimbali za mikopo ya muda mfupi ili kuimarisha biashara zao kwa ufanisi, urahisi na uhakika.

"Dhamira yetu ni kutoa mitaji kwa wajasiriamali wa kilimo itakayosaidia kustawi kwa sekta ya kilimo. Mikopo hii imeundwa kwa kusudi la kusaidia gharama za mavuno, gharama za usindikaji na gharama za maghala/kodi za maghala, ili wajasiriamali wanufaike zaidi katika shughuli zao," alisema.

Macharo alisema wajasiriamali wanaweza kupata mikopo kuanzia Sh. 100,000 hadi Sh. milioni moja kwa mtu binafsi au kikundi kulingana na mahitaji yao.

Alisema kiasi hicho kinaweza kutolewa kwa njia ya simu ya mwombaji ili kurahisisha malipo ya fedha kwa wakati na hata kurahisisha urejeshwaji wake kwa njia hiyo hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa PASS Trust, Yohane Kaduma, alisema wanaamini sekta hiyo ndiyo nguzo ya uchumi wa nchi. Ushirikiano wao ni ushuhuda tosha wa kusaidia sekta hiyo.

"Ndiyo maana sisi PASS, tunatoa dhamana za mikopo ya kidijitali kupitia simu za mkononi, kuruhusu wakulima kupata huduma hiyo, kutoka kwa taasisi za kifedha tukianza na Taasisi ya Victoria Finance.

"Ushirikiano huu kati ya PASS na Victoria Finance unaonesha dhamira ya kuendelea kuwawezesha wajasiriamali wa kilimo, kukuza mnyororo wa thamani wa kilimo na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi ya Tanzania," alisema Kaduma.

Alibainisha kuwa wamekuwa wakitoa dhamana ya mikopo ya kilimobiashara ili kuwawezesha wajasiriamali kuepukana na changamoto ya kukosa mitaji na fedha za kukamilisha mahitaji yao kwa wakati.

"Hadi sasa takribani miradi 72,201 imedhaminiwa na PASS Trust. Mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 1.5 imetolewa kwa wajasiriamali wa kilimo biashara. Vilevile, ajira takribani milioni 2.7 zimetengenezwa kutokana na huduma zetu," alitamba.

Victoria Finance ni taasisi ya kifedha inayowezesha mahitaji ya kifedha kwa wakulima wadogo, biashara ndogo na za kati na wajasiriamali walio katika mnyororo wa thamani wa kilimo nchini.

# Wafanyabiashara washauriwa kutumia teknolojia ya China kuanzisha viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wa Tanzania wanaosafiri na kuagiza bidhaa kutoka China, wameshauriwa kutumia vyema ushirikiano baina ya mataifa hayo mawili kwa kuangalia namna ya kutumia teknolojia ya China kuanzisha viwanda nchini badala ya kujikita kuagiza bidhaa kutoka China.

Konseli Mkuu wa Ubalozi Mdogo wa Tanzania jijini Guangzhou, China, Khatib Makenga, ametoa rai hiyo alipozungumza na kundi la wafanyabiashara kutoka maeneo mbalimbali nchini waliopata fursa ya kwenda China kushiriki Maonyesho ya Uagizaji na Uuzaji wa Bidhaa za China.

Wafanyabiashara hao wamepata fursa hiyo kwa uratibu wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kupitia klabu yake ya biashara (NBC B-Club).

Akiwasilisha wito wa konseli huyo mbele ya waandishi wa habari baada ya kurejea nchini mwishoni mwa wiki, Meneja Bidhaa na Huduma za Kibenki wa NBC, Jonathan Bitababaje, aliyeongoza wafanyabiashara hao, aliwasilisha rai hiyo.

Alisema kuwa katika mazungumzo yao na konseli huyo, mbali na kuipongeza benki hiyo kwa hatua hiyo muhimu, aliwasisitiza Watanzania kutumia vyema ushirikiano baina ya mataifa hayo mawili kwa kuwa na maono ya kuanzisha viwanda Tanzania badala ya kutegemea tu kuagiza bidhaa kutoka China.

"Kwa mujibu wa Mheshimiwa Konseli, China kuna teknolojia za ukubwa tofauti, hivyo Watanzania wana fursa ya kuangalia teknolojia wanazozimudu ikiwamo teknolojia rahisi itakayowawezesha kuzalisha baadhi ya bidhaa ndogondogo hapahapa nchini ili kupunguza idadi ya bidhaa zinazoingizwa kutoka China," alisema Bitababaje.

Alibainisha kuwa benki hiyo iko tayari kuwasaidia wafanyabiashara hao kwa kuwapatia mitaji itakayowasaidia kutimiza kwa vitendo yale yote waliyojifunza China.

Kupitia safari hiyo ya siku 10, wafanyabiashara hao walipata fursa ya kujifunza mambo mengi ikiwamo fursa za biashara, uwekezaji na ushirikiano wa kibiashara huku pia wakipata fursa ya kutembelea viwanda na masoko mbalimbali.

Wakiwa njiani kuelekea na kurudi katika safari hiyo, wafanyabiashara hao pia walipata wasaa wa kutembelea nchi ya Misri na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii na historia ya taifa hilo.

"Zaidi, tukiwa China, tulipata fursa ya kukutana na wafanyabiashara wakubwa, wamiliki wa viwanda vikubwa na vidogo. Pia wafanyabiashara waliweza kujifunza teknolojia mpya sambamba na kupata muunganiko mpya wa kibiashara na wenzao kutoka China.

"Kuna ambao walihitaji mashine na zana mbalimbali kwa ajili ya kazi zao wamepata na pia wapo waliopata washirika wapya kibiashara. Ni matumaini yetu kwamba hivi karibuni tutashuhudia uwekezaji wao mpya kupitia viwanda.

"Niwaombe sana wafanyabiashara waendelee kuchangamkia fursa ya safari hizi ambazo zinaendelea kuja kupitia uratibu wa NBC B-Club ambapo tunatarajia kuwa na safari nyingine za China mwezi Aprili na Oktoba mwakani.

"Mbali na China, pia tutakuwa na safari za Ulaya, Asia na baadhi ya nchi za Afrika ambazo tuna ushirikiano mkubwa wa kibiashara," alisema.

Wakizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wengine waliopata fursa hiyo, Renatus Porini na Sarah Munuo, mbali na kuishukuru benki hiyo kwa uratibu wa safari hiyo, walisema wamejifunza mambo mengi ikiwamo fursa mpya nyingi za kimasoko na uhusiano wa biashara, hatua ambayo imewajenga zaidi kibiashara.

"Kimsigi, tulivyorudi leo si kama tulivyokwenda! Tukiwa China na Misri tulitembelea maeneo mbalimbali vikiwamo viwanda na pia tumeongeza mawasiliano zaidi na wenzetu wa huko China," alisema Porini.

# Mtanzania aeleza 'kutoweka' mtoto wake Israel kwa siku 18

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni karibu wiki ya tatu sasa tangu kikundi cha Hamas kuivamia Israel, Mtanzania Loitu Mollel ambaye ni baba mzazi wa Joshua Loitu (Pichani) anayeishi Israel, amedai hana mawasiliano na mwanawe licha ya kufanya jitihada mbalimbali za kumtafuta.

Mollel ambaye alizungumza na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) jana, alisema mara ya mwisho kuwasiliana na mwanawe huyo ilikuwa Oktoba 5 mwaka huu na mara ya mwisho mawasiliano yake 'yako hai' (online) mtandaoni ilikuwa Oktoba 7 mwaka huu saa 4:03 asubuhi, jambo linalomfanya akose furaha.



Hatua ya kufuatilia aliko mwanawe inakuja siku kadhaa baada ya Ubalozi wa Tanzania nchini Israel kusema kuwa hauna mawasiliano na Watanzania wawili ambao wanaishi eneo la kusini mwa nchi hiyo ambalo lilishuhudia mapambano baina ya wanamgambo wa Kipalestina wa Hamas na Jeshi la Israel.

"Sifahamu kuwa Joshua yuko katika hali gani na ninasubiri taarifa kutoka kwenye mamlaka za Tanzania. Sina furaha, familia haina furaha kwa sababu hatumpati kwenye simu huyu kijana, mke wangu na ndugu zangu wanataka niongeze jitihada ili kufahamu aliko na yuko katika hali gani.

"Jitihada ninazoendelea nazo ni kufuatilia kupitia kwa Ubalozi wa Tanzania nchini Israel licha ya kuwa na wao wamenieleza kuwa wanaendelea kufuatilia kufahamu aliko kijana wangu," alisema Mollel.

Alibainisha kuwa Joshua alikwenda Israel Septemba 18 mwaka jana kwa ajili ya masomo kwa vitendo.

Hata hivyo, mpaka jana Ubalozi wa Tanzania huko Israel ulisema kuwa haujafanikiwa kuwasiliana na vijana ambao ulieleza awali kwamba haukuwa na mawasiliano nao.

Vilevile, hivi karibuni, Ubalozi wa Tanzania nchini Israel uliwarudisha Watanzania tisa waliokuwa nchini humo, huku wengine zaidi ya 350 wakiendelea kuishi katika maeneo mbalimbali nchini Israel.

**BBC**

# 'Mitandao ya jamii itumike kutoa elimu ya kodi nchini'

**Na Joseph Mahumi,** MOROGORO

MKUU wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Fedha, amewataka wadau wa mitandao ya kijamii kuwa mstari wa mbele kuelimisha jamii umuhimu wa kulipa kodi na kudai risiti halali zinazolingana na kiasi cha fedha walichotoa kila wanapofanya ununuzi na kutoa risiti wanapouza bidhaa na huduma.

Benny Mwaipaja alitoa rai hiyo jana wakati akifungua Kongamano la Wadau wa Mitandao ya Kijamii na Wizara ya Fedha linalofanyika mkoani Morogoro kwa siku mbili kuanzia jana.

Alisema mitandao ya kijamii imekuwa njia ya kidijitali ya kuifikia jamii kwa haraka na kwa ukubwa, akiwaomba wadau hao kutumia fursa hiyo kuielimisha jamii umuhimu wa kulipa kodi ili kusaidia kukuza uchumi wa nchi na kuleta maendeleo kwa wananchi.

"Wizara inawatambua ninyi ni wadau muhimu sana. Ninaomba mkawe vinara wa kuelimisha jamii ili kuongeza elimu ya masuala ya kodi na kuelezea kazi nzuri inayofanywa na serikali katika kusimamia uchumi na pia kuwaelimisha jamii kuhusu agenda ya maendeleo ya taifa na miradi inayotekelezwa na serikali kwa ajili ya maslahi ya Watanzania ikiwamo miradi ya kimkakati, alisema.

Mwenyekiti wa kongamano hilo, Mathias Canal aliipongeza wizara ya fedha kwa kuandaa kongamano hilo. Ni fursa ya kurahisisha utendaji kazi wao kwa umma hasa kwa kujengewa uwezo kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Wizara ya Fedha.

Canal aliongeza kuwa Wizara ya Fedha iendelee kutoa ufafanuzi kwa umma kuhusu miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali na umuhimu wa mikopo ili kuondoa sintofahamu kwa jamii kuhusu mikopo ya serikali.

"Hongera sana Mkuu wa Kitengo cha Habari Wizara ya Fedha, Benny Mwaipaja, kwa kubuni kongamano hili, pia tufikishie salamu za pongezi kwa Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba kwa kukubali kufanyika kwa kongamano hili ambalo ni muhimu kwa wadau wanaohabarisha jamii," alisema.

Kongamano hilo la siku mbili linatoa fursa kwa wadau wa mitandao ya kijamii kujifunza masuala mbalimbali kuhusu wizara hiyo na kujengewa uwezo kuhusu katika masuala ya sheria mpya ya PPP, muundo wa wizara, Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha nchini na masuala ya pensheni.





airtel
A REASON TO IMAGINE

MUONGOZO WA GHARAMA ZA AIRTEL KUANZIA OKTOBA - DISEMBA 2023

**LIPIA KADRI UNAVYOTUMIA: KODI IMEJUMUISHWA**

| | | Bei (TSh) |
|---|---|---|
| MITANDAO YOTE | TSh / sek | 0.50 |
| NDANI YA MTANDAO | TSh / sek | 0.50 |
| INTANETI | TSh / Mb | 9.35 |
| SMS ZA NDANI YA NCHI | TSh / Sms | 8.00 |
| SMS ZA NJE YA NCHI | TSh / Sms | 215.00 |

**MITANDAO YOTE**

| Muda | Bei(TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS |
|---|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 30 | 25 |
| Saa 48 | 1,000 | 150 | 25 |
| Siku 7 | 1,500 | 150 | 50 |
| Siku 7 | 2,500 | 300 | 50 |
| Siku 30 | 5,000 | 400 | 100 |
| Siku 30 | 10,000 | 1,200 | 100 |

**BANDO ZA SMS**

| Muda | Bei(TSh) | SMS |
|---|---|---|
| Saa 24 | 200 | 200 |
| Siku 7 | 500 | 1,000 |
| Siku 30 | 1,000 | 10,000 |

**BANDO ZA INTANETI**

| Muda | Bei (TSh) | Intaneti (MB) |
|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 246 |
| Saa 24 | 1,000 | 492 |
| Siku 3 | 2,000 | 985 |
| Siku 7 | 2,000 | 950 |
| Siku 7 | 2,100 | 1,024 |
| Siku 7 | 3,000 | 1,480 |
| Siku 7 | 5,000 | 2,460 |
| Siku 30 | 10,000 | 4,920 |
| Siku 30 | 20,000 | 9,850 |
| Siku 30 | 30,000 | 14,780 |
| Siku 60 | 50,000 | 24,600 |
| Siku 60 | 100,000 | 49,200 |

**BANDO ZA AIRTEL - AIRTEL**

| Muda | Bei (TSh) | Ndani ya Mtandao (Dak) | Mitandao Yote (Dak) | SMS |
|---|---|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 90 | 10 | 25 |
| Saa 48 | 1,000 | 260 | 40 | 25 |
| Siku 7 | 1,500 | 260 | 40 | 50 |
| Siku 30 | 5,000 | 1,000 | 250 | 100 |

**COMBO (DAKIKA + MB)**

| Muda | Bei (TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS | Intaneti(MB) |
|---|---|---|---|---|
| Saa 24 | 1,000 | 40 | 10 | 350 |
| Siku 7 | 2,000 | 55 | 10 | 800 |
| Siku 30 | 10,000 | 400 | 10 | 3,600 |
| Siku 30 | 20,000 | 500 | 10 | 8,192 |

**BILA KIKOMO**

| Muda | Bei (TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS | Intaneti (MB) |
|---|---|---|---|---|
| BILA KIKOMO | 1,000 | 60 | 50 | |
| BILA KIKOMO | 2,000 | 20 | | 900 |

**MUONGOZO WA GHARAMA ZA KIMATAIFA (KODI HAIJAJUMUISHWA)**

| Nchi | BAND | Bei(TSh/Sek) |
|---|---|---|
| China, Canada, India, USA | Band 1 | 8 |
| Malaysia, Japan, Lebanon, Ethiopia, Nigeria, Pakistan, Yemen, Sudan, Kenya Airtel, Kenya Other Network, United Arab Emirates | Band 3 | 10 |
| REST OF AFRICA, Denmark, Germany, Ireland, Netherlands, Norway, Spain, Sweden, Oman, Italy, Ghana | Band 5 | 14 |
| Zambia, Dem. Rep. of Congo, Zimbabwe, Burundi, Malawi | Band 6 | 25 |
| France, Rest of World, South Africa, United Kingdom | Band 7 | 13 |
| Central African Republic, Sao Tome & Principe, San Marino, Montenegro, Cuba, Martinique, East Timor, Nauru, Papua New Guinea, Solomon Islands, Vanuatu, Wallis & Fatuna, Cook Islands, Kiribati, Tuvalu, Micronesia, Maldives, South Sudan, Comoros, Gambia, Latvia, Somalia, Bulgaria, Lithuania, Moldova, Albania, Belarus, Congo, Guinea, Guinea Bissau, Seychelles, Sierra Leone, Senegal, Samoa, Tonga, Uzbekistan, Vanautu, Cameroon, Chad, Gabon, Madagascar, Belgium, Switzerland | Band 8 | 47 |
| Uganda , Uganda celtel, Rwanda | Band 11 | 15 |
| Satellite, Inmarsat, Premium Diego Garcia, Ascension Island, St.Helena, GreenLand Falkland Islands, Tokelau, Dem. Rep. Of Congo, Special numbers, Chile, Australia Territories, Niue Island, Upt, Norfolk Island, Chile | Band 12 | 233 |

| BANDO ZA KIMATAIFA | MUDA | BEI YA BANDO (TSH) | DAKIKA |
|---|---|---|---|
| INDIA, CHINA, USA CANADA | Saa 24 | 1,000 | 20 |
| AFRIKA KUSINI | Saa 24 | 3,000 | 5 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Saa 24 | 2,500 | 5 |
| ULAYA | Saa 24 | 2,500 | 4 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Saa 24 | 2,500 | 3 |
| INDIA, CHINA, USA CANADA | Siku 7 | 5,000 | 100 |
| AFRIKA KUSINI | Siku 7 | 6,000 | 10 |
| MALAWI, DRC | Siku 7 | 10,000 | 8 |
| ZAMBIA | Siku 7 | 10,000 | 9 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Siku 7 | 5,000 | 10 |
| UK, ITALY, GERMANY | Siku 7 | 5,000 | 8 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Siku 7 | 5,000 | 6 |
| INDIA, CHINA, USA CANADA | Siku 30 | 15,000 | 300 |
| AFRIKA KUSINI | Siku 30 | 15,000 | 25 |
| MALAWI, DRC | Siku 30 | 20,000 | 16 |
| ZAMBIA | Siku 30 | 20,000 | 18 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Siku 30 | 15,000 | 30 |
| UK, ITALY, GERMANY | Siku 30 | 15,000 | 24 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Siku 30 | 15,000 | 18 |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | Dakika za kupiga simu | Dakika za kupokea simu | MB |
|---|---|---|---|---|---|
| Eneo -1 | Siku 3 | 10,000 | 5 | 5 | 75 |
| Eneo -1 | Siku 7 | 25,000 | 15 | 10 | 250 |
| Eneo -1 | Siku 14 | 40,000 | 25 | 20 | 500 |
| Eneo -2 | Siku 3 | 25,000 | 12 | | 250 |
| Eneo -2 | Siku 7 | 50,000 | 15 | | 200 |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo -1 | Saa 24 | 5,000 | 500 |
| Eneo -1 | Siku 3 | 10,000 | 1,299 |
| Eneo -1 | Siku 7 | 15,000 | 2,048 |
| Eneo -1 | Siku 14 | 30,000 | 5,120 |

**SAFARI ROAMING BANDO - KUPIGA NA KUPOKEA SIMU**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | Dakika za kupiga simu | Dakika za kupokea simu |
|---|---|---|---|---|
| Eneo -2 | Siku 7 | 10,000 | 10 | |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo -3 | Siku 3 | 40,000 | 1024 |
| Eneo -3 | Siku 7 | 75,000 | 2048 |
| Eneo -3 | Siku 14 | 200,000 | 5120 |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo - 4 | Siku 3 | 35,000 | 200 |
| Eneo - 4 | Siku 7 | 90,000 | 512 |
| Eneo - 4 | Siku 14 | 175,000 | 1024 |

| | |
|---|---|
| **Eneo 1** | Kongo B(Airtel), DRC(Airtel), Gabon(Airtel), Ghana(Airtel),Kenya(Airtel), Madagasca(Airtel), Malawi(Airtel), Niger(Airtel), Nigeria(Airtel), Rwanda(Airtel), Seychelles(Airtel), Tchad(Airtel), Uganda(Airtel), Zambia(Airtel), India(Airtel) & Mauritius(Emtel) |
| **Eneo 2** | **AFRIKA:** Botswana(MTN), KongoB(Airtel), KongoDRC(Airtel), Egypt(Orange), Gabon(Airtel), Ghana(Airtel), Kenya(Airtel), Madagascar(Airtel), Malawi(Airtel), Mauritius(Emtel), Mozambique(Vodafone), Niger(Airtel), Nigeria(Airtel), Rwanda(Airtel), Afrika Kusini (MTN, Vodafone), Swaziland(MTN), Tchad(Airtel), Uganda(Airtel), Zambia(Airtel) |
| | **MAREKANI:** (T-Mobile) & CANADA: (Bell, Telus) |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** China(China Mobile), Bangladesh(Airtel), India(Airtel), Israel(Pelephone, Cellcom), Oman(OmanTel), Pakistan(Telenor, Vimplecom), Qatar(Qtel), SaudiArabia(Zain), SriLanka(Airtel), Turkey(Vodafone), UAE (dU, Etisalat) |
| | **ULAYA:** Denmark(Telenor, TDC), France(Orange, SFR), Germany(T-Mobile, Vodafone), Greece(T-Mobile), Italy(Vodafone,Tim), Netherlands(Vodafone, KPN), Norway(Telenor), Romania(Vodafone, Orange), Russia(Vimpel-com), Spain(Vodafone, Telefonica), Sweden(Telenor), UK(Vodafone,Telefonica) |
| | **OCEANIA**: New Zealand(Vodafone) |
| **Eneo 3** | **AFRIKA:** Botswana(MTN), Cameroun(Orange), Egypt(Orange), Ghana(Airtel, TIGO), Mali(Orange), Mozambique(Vodacom), Mauritius(Emtel), Senegal (Orange), Swaziland(MTN), Afrika Kusini(MTN, Vodacom) |
| | **MAREKANI:** (T-Mobile) & CANADA: (Bell, Telus) |
| | **ULAYA:** Belgium(Base, Orange), Switzerland(Swisscom), Denmark(Telenor, TDC), France(Orange, SFR), Germany(T-Mobile, Vodafone), Greece(Cosmote), Italy(Vodafone,Tim), Netherlands(Vodafone, KPN), Norway(Telenor), Romania(Vodafone, Orange), Russia(Vimpelcom), Spain(Vodafone, Telefonica), Sweden(Telenor), UK(Vodafone,Telefonica) |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** India(Airtel), Israel(Orange, Pelephone, Cellcom),Pakistan(Mobilink, Telenor), Qatar(Qtel), SaudiArabia(Zain), Sri Lanka(Airtel), Turkey(Vodafone), UAE(Etisalat) |
| | **CHINA:** China Mobile |
| **Eneo 4** | **AFRIKA: Afrika Kusini**(Cell C) |
| | **MAREKANI:** AT&T |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** Oman (OmanTel), UAE (dU), Turkey (Turkcel) |

*Vigezo na masharti kuzingatiwa. Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu: https://www.airtel.co.tz

217663602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madereva kuweni makini ajali zinamaliza nguvukazi

**WIKI** iliyopita kulitokea ajali iliyosababisha vifo vya watu wengi mkoani Tabora na chanzo kinaelezwa kuwa ni uzembe wa dereva.

Ajali hiyo ilitokea Oktoba 20, mwaka huu saa tano asubuhi katika eneo la Udomouchana, wilayani Nzega ilihusisha basi la abiria na lori la mafuta na kuua watu 18 huku wengine 35 wakijeruhiwa.

Imeelezwa kuwa ajali hiyo imesababishwa na uzembe wa dereva wa lori la mafuta lililokuwa likitokea Dar es Salaam kwenda mkoani Mwanza baada ya dereva huyo kuchepuka (overtaking) bila kuchukua tahadhari na kuligonga basi lililokuwa likitokea Mwanza kuelekea Dar es Salaam.

Ajali zinazosababishwa na madereva 'ku-overtake' magari mengine bila hata kuchukua tahadhari, zimekuwa zikitokea mara kwa mara na kuua watu wengi.

Madereva wa mabasi ya mikoani ndio wanaoongoza kwa kuyapita magari mengine tena zaidi ya moja bila kujali yuko kwenye eneo lenye kona, mteremko au kwenye mlima.

Abiria wanapolalamika dereva anapokiuka sheria za usalama barabarani, anaweza kuambiwa ateremke kwenye basi au apande usafiri wake binafsi.

Katika ajali iliyotokea mkoani Tabora, Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, alithibitisha kutokea vifo vya watu 18 na wengine 35 waliojeruhiwa kupelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega kwa ajili ya matibabu zaidi.

Waliofariki kwenye ajali hiyo 13 ni wanaume na watano ni wanawake.

Ukiangalia waliofariki kwenye ajali hiyo wengi ni watu waliokuwa wakitegemewa na familia zao na taifa katika uzalishaji.

Nguvukazi yote hiyo inayopotea maana yake ni taifa limeingia hasara ya kupoteza rasilimali watu na vilevile familia za watu walipoteza maisha zinabaki kwenye wakati mgumu.

Ajali zinapotokea husababisha mambo mengi, pamoja na vifo kuna uharibifu wa mali, miundombinu ya barabara na wamiliki wa vyombo hivyo vya usafiri kuingia hasara.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tabora, ajali hiyo imesababishwa na mwendo kasi na uzembe wa dereva wa lori ambaye alichepuka bila kuchukua tahadhari na kuligonga basi.

Licha ya tahadhari za vibao vinavyoelekeza madereva kuvifuata ili kuepuka ajali, bado kuna baadhi yao hupuuza kwa kujiona welevu zaidi barabarani.

Madereva ni lazima waendelee kufuata sheria za barabarani na kuacha kuendesha kwa mazoea kwa sababu kufanya hivyo ni kinyume cha sheria na kanuni za barabarani na kumekuwa kukigharimu maisha ya Watanzania wengi.

Baadhi watu walioshuhuda ajali hiyo walieleza kuwa lori la mafuta lilionekana kuwa katika mwendokasi na wakati wa kupishana likapoteza mwelekeo na kulikagonga basi hilo upande wa kushoto wa dereva.

Madereva wanaoendesha magari makubwa baadhi yao hujifanya kama ni watawala wa barabara na kwamba wao ndio wenye haki ya kufanya wanavyotaka huku wakitunishia misuli madereva wa magari madogo.

Pia madereva hao wanaposababisha ajali hukimbia na kutokomea kusikojulikana huku wakiacha maisha ya watu wasiokuwa na hatia yakiteketea.

Wakati umefika sasa, madereva wanaosababisha ajali kwa sababu ya uzembe wachukuliwe hatua kali, ikiwamo kufungiwa kabisa kuendesha vyombo vya moto ili kutoa fundisho kwa wengine wenye kuleta jeuri na kupoteza nguvukazi za taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Wazalisha umeme zipo fursa TIB

**BENKI** ya Maendeleo Tanzania (TIB) imetangaza mipango na mikakati kwa kipindi cha miaka mitano kwa ni pamoja na kutoa mkopo kwa Watanzania wabobezi wa sayansi wanaozalisha umeme jadidifu vijijini.

Inalenga ambako umeme TANESCO haufiki ili kuwanufaisha wananchi wengi zaidi badala ya wanaoishi mjini pekee, kuufurahi na kubadili maisha yao.

Mpango huo unatangazwa na Kaimu Mkurugenzi wa TIB, Lillian Mbassi, anapozungumza na wanahabari hivi karibuni.

Kaimu Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa hatua hiyo ya kukopesha wazalishaji hao wa umeme jadidifu kupitia dirisha maalum lilipo katika benki hiyo, ni miongoni mwa mipango na mikakati ya TIB katika kipindi cha kuanzia 2021 hadi mwaka 2025.

Anasema mpango huo unaenda sambamba na kupanua huduma ya kusambaza umeme vijijini kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), ambao ni wadau wakubwa wa benki hiyo katika kupelekea huduma muhimu wananchi wanaoishi vijijini.

Anataja mikakati mingine ya BIT kuwa ni kuunga mkono jitihada za serikali kutekeleza sera na mikakati ya kitaifa ili kuongeza kasi ya maendeleo kwa wananchi.

Mpango huo wa TIB una lengo la kuwawezesha Watanzania ambao wamejitokeza kutangaza teknolojia zao za kuzalisha umeme kwa njia mbalimbali ambao wamekuwa wakihitaji msaada wa fedha kutoka kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi ili kutimiza ndoto zao kuzalisha umeme kwa ajili ya matumizi ya nyumba, ofisini na taasisi nyingine zinazotoa huduma kwa umma.

**Mpango huo unatangazwa na Kaimu Mkurugenzi wa TIB, Lillian Mbassi, anapozungumza na wanahabari hivi karibuni.**

Miongoni mwa hao ni mkazi wa Dar es Salaam, ambaye amejitokeza akisema anahitaji msaada wa fedha ili aweze kukamilisha ujenzi wa mradi wake wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya kisima cha kuchimba na wala si mabwawa wala mito ambayo kila mara hukauka.

Anasema mtambo wake wa kuzalisha umeme ambao ameupa jina la 'tanzanite' unafua nishati hiyo kwa maji ambayo yanahifadhiwa kwenye kisima na ni umeme wa uhakika kwani unapatikana kwa wakati wote.

TIB kwa kuwa wametangaza fursa hiyo kwa wanasayansi kama huyo na wengine wana kila sababu ya kujitokeza ili kukopeshwa fedha na kutimiza ndoto zao kupeleka nishati yao hiyo katika maeneo ya vijijini ambako umeme unaozalishwa na TANESCO haufiki na kuwa mkombozi kwa wananchi kuacha kutumia taa za chemli, vibatari na moto wa kuni kupata mwanga nyakati za usiku.

Nishati hiyo jadidifu, pia itawasaidia wananchi wa vijijini kubadili mfumo wao wa maisha kutoka waliyoyazoea na kuwa wa kisasa zaidi kwa kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanaendelea kutokea duniani katika kipindi hiki cha utandawazi.

Si jambo geni kusikia kwamba kuna vijiji tangu Uhuru hadi leo havijawahi kuwa na umeme na watu wake wanasikia tu kuwepo kwa nishati hiyo na wengine wanashuhudia wakifika mijini au vijiji jirani.

Vijiji kama hivyo, ni kama viko katika ulimwengu mwingine wa giza kwani havina mawasiliano ya simu, runinga, wala mitandao ya intaneti ambayo ni mpango mzima wa maisha ya mwanadamu kwa kupata taarifa mbalimbali kutoka kwa ndugu, jamaa au kwa kusikiliza na kufuatilia habari kutoka sehemu zote bila kizuizi.

Wenye teknolojia hiyo wasibweteke, TIB imewaonyesha njia za kupata fedha kwa kuwapa mkopo, ikiwa watafuata taratibu kama ambavyo wengine walivyofanya kwenye sekta ya kilimo kwa kufanya uwekezaji na kutoa ajira kwa watu 10,000.

Kulingana na Mkurugenzi Mbassi, watu hao 10,000 ni kati ya 30,000 waliopata ajira kwenye miradi ambayo imewezeshwa kwa mikopo iliyotoa kwa wawekezaji.

HABARI KITAIFA

# Taasisi za fedha zilivyojipanga tishio El-Nino

**Na Jenifer Gilla**

TAASISI za fedha nchini zimeeleza namna zilivyojiandaa kuboresha huduma za kifedha ili kuwaepusha wateja wao na athari za mvua kubwa (El-Nino) iliyotangazwa na Mamlaka ya Hali Hewa nchini (TMA).

Mamlaka hiyo imetahadharisha uwezekano wa El-Nino nchini kuanzia mwishoni mwa mwezi huu hadi Desemba mwaka huu, hivyo kutoa hadhari ya madhara kwa binadamu na mazingira ikiwamo vifo, mafuriko, ardhi kuporomoka, upotevu wa mali, magonjwa ya mlipuko na uharibifu wa miundombinu, hivyo kuwataka wananchi kuchukua tahadhari.

Kutokana na angalizo hilo la TMA, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) nayo imezitahadharisha taasisi za fedha kuhusu madhara yatokanayo na mvua hiyo.

BoT imeelekeza taasisi hizo kuchukua hatua zinazofaa ili kupunguza changamoto za huduma za kifedha katika kipindi hicho ikiwamo kuweka akiba ya kutosha ya fedha taslimu katika vyumba vya kuhifadhi fedha.

Benki Kuu pia imeshaelekeza taasisi za fedha kuhimiza wateja kutumia mifumo ya kielektroniki kufanya malipo na kudumisha huduma ya mtandao ili kuwezesha wateja kufanya miamala na kuongeza kiwango cha mwisho cha kufanya miamala kwa siku.

BoT pia imezielekeza kufanya tathmini ya utayari wa mipango ya kurejesha biashara na teknolojia ya habari na kuhakikisha akaunti za mfumo wa malipo ya papo hapo wa Tanzania zinafadhiliwa vya kutosha.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Godwin Semunyu, alipozungumzia hatua wanazochukua kama tahadhari ya El-Nino, anasema wanaendelea kutoa elimu kwa wateja kuhusu ujio wa mvua hizo na kuwaelekeza kujikita zaidi kujihudumia kwa kutumia simu (Simbanking).

Anasema pia wanawaelekeza wateja kutumia mawakala wa benki hiyo walioko karibu nao kupata huduma za kifedha pamoja na kutatuliwa changamoto za kawaida za kifedha badala ya kutumia muda mrefu kwenda benki.

"Tunawaelimisha hivyo ili kuwaepusha na madhara yatokanayo na mvua hizo kwa sababu tunajua historia yake, mara nyingi inasababisha uharibifu wa miundombinu ikiwamo madaraja kujaa maji na kukatika. Sasa tusingependa kusikia mteja wetu kapata madhara akitafuta huduma yetu," alisema.

Semunyu pia alisema wameboresha huduma za kimtandao ili sizilete shida katika kipindi hicho ambacho wateja watakuwa wanazitumia zaidi kujipatia huduma za kifedha.

Mkuu wa Usalama wa Kampuni na Uendelevu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Misana Mutani, anasema wamejipanga kukabiliana na athari za mvua hiyo kwa kuchukua hatua kadhaa muhimu ikiwamo kuhuisha menejimenti kudhibiti majanga na kuiweka tayari kwa timu ya kukabili majanga pindi yatakapojitokeza.

Anasema wanazifanyia majaribio huduma na bidhaa zao zote muhimu zikiwamo mashine za kutolea fedha (ATM), mawakala, huduma za benki kupitia simu za mkononi na mtandao ili wateja wajihudumie wakiwa nyumbani. Mutani anatoa wito kwa wateja wao na Watanzania kwa ujumla kuwa makini na watulivu katika kipindi hicho cha mvua ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza na kufuatilia taarifa za mamlaka husika tahadhari zitakazokuwa zinatolewa.

Anawaomba wateja ikitokea changamoto yoyote pindi wanapohitaji huduma ya kibenki, wawasiliane na idara ya huduma kwa wateja kwa njia ya simu badala ya kutembea umbali mrefu kwenda benki na kujiweka katika hatari ya kuathiriwa na majanga yatakayotokana na mvua hizo.

Mkurugenzi wa taasisi ya mikopo ya Madeo Finance, Shaba Kilasi, anasema wanashirikiana na taasisi zingine za fedha kama vile mitandao ya simu kuwawekea wateja mfumo wa kulipa marejesho kwa njia ya kielektroniki.

Anasema pia wanatoa elimu kwa wateja namna ya kufanya miamala ya kulipa marejesho kwa njia ya kielektroniki kama vile kutumia lipa namba za mitandao ya simu ili kuwaepusha na hatari ya kuathiriwa na mvua hizo kwa kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo katika matawi yao.

Julai 19 mwaka huu, TMA ilitoa tahadhari ya mvua ya El-Nino msimu wa vuli katika mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka ikiwamo maeneo ya mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza na Shinyanga.

Maeneo mengine yenye uwezekazo wa kupata mvua hiyo ni Simiyu, kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma, Dar es Salaam, Tanga, Pwani na kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro. Wananchi wachukue tahadhari.

Agosti 31 mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alielekeza kamati za usimamizi wa maafa na sekta, kushirikiana na umma kuchukua baadhi ya hatua kama vile kutambua maeneo hatarishi na yenye viashiria vya kuathirika na maafa.

Jenista pia alizielekeza kamati hizo kuandaa mipango ya kuzuia madhara na kukabiliana na maafa endapo yatatokea, pia kuainisha na kuandaa rasilimali za usimamizi wa maafa kwa kila sekta kushiriki kikamilifu katika eneo lake.

"Tunazielekeza kamati hizo zisisubiri maafa yatokee, waanze kutambua maeneo yote hatarishi na yenye viashiria vya kuathirika na maafa na kuanza kuandaa mipango ya kuzuia madhara yoyote yanayoweza kutokea kulingana na utabiri huo wa TMA," aliagiza waziri huyo.

# SMZ yajenga hospitali wilaya, yabinafsisha uendeshaji wake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR



RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali yake imejenga hospitali ya wilaya, ambayo imeamua kuiwekeza katika mfumo binafsi, ili kupata ufanisi katika uendeshaji wake.

Ni kauli yake Rais Dk. Mwinyi, ambaye kitaaluma ni daktari wa binadamu, alipofungua Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini A Unguja iliyojengwa hivi karibuni huko Kivunge.

Kwa mujibu wa Rais Mwinyi, hospitali hiyo ni miongoni mwa 10 za wilaya zilizojengwa kupitia fedha za Mpango wa Kukabiliana na Athari za UVIKO-19 zilizotolewa kupitia mkopo wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Dk. Mwinyi alisema baadhi ya watu hawapendi mageuzi hayo ambayo yanasaidia katika utoaji huduma bora na haraka kwa wananchi.

Alisema serikali haitokuwa tayari kuona huduma za afya zinadorora baada ya kushirikisha sekta binafsi.

"Kwanini tumefanya hivi kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa maabara katika hospitali? Mara kadhaa imetokea katika hospitali za serikali ambapo kifaa kinakuwa kimeharibika, lakini utaratibu wetu wa serikali unataka ufuate sheria ya ununuzi na huchukua muda mrefu hadi kukamilika na huwaumiza watu, hakuna mgonjwa anayeweza kusubiri mpaka utaratibu wa ununuzi ukamilike," alifafanua.

Dk. Mwinyi alitoa indhari kwa sekta binafsi zilizopewa kazi katika sekta ya afya kuhakikisha kutoa huduma bora, za kisasa na haraka. Serikali haitokuwa tayari kuona ucheleweshaji utoaji huduma.

"Tuliowapa kazi ya kuendesha hospitali hizi tunataka wahakikishe dawa zote zinapatikana. Pamoja na hayo, kuna huduma ambazo si za kitabibu zinafanywa na sekta binafsi ili tupate ufanisi zaidi," alisema.

Rais Dk. Mwinyi alisema ameshatoa maelekezo kwa huduma ambazo si za kitaalamu, ikiwamo masuala ya usafi kuwachukua vijana wazawa kufanya kazi hizo.

Aliwataka wafanyakazi wa serikali katika sekta ya afya kutokuwa na wasiwasi na utaratibu huo mpya kwa kuwa una dhamira njema ya kufanya huduma za afya kuwa bora na si vinginevyo.

"Wafanyakazi wa serikali ninawatoeni hofu mabadiliko haya hayamtoi yeyote katika ajira yake na mtabaki katika ajira zenu na kikubwa zaidi mtapata ujuzi zaidi. Wala hamna haja ya kuwa na hofu, mtaendelea kulipwa na serikali wala hakuna shida yoyote," alifafanua.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali imeamua kufanya huduma za afya kuwa bora na ili ziwe bora, lazima kujenga mfumo wa rufani ili kuipunguzia mzigo mkubwa hospitali kuu ya Mnazi mmoja.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema Wilaya ya Kaskazini A Unguja ina wakazi 162,000, vituo vya afya ngazi ya msingi 15, hospitali binafsi 15 na maduka ya dawa ya watu binafsi 11.

Alisema kwa kipindi cha mwaka jana pekee, Hospitali ya Kivunge ilitoa huduma za uzazi kwa kinamama 4,425 na kutoka Januari hadi Septemba mwaka huu imetoa huduma hizo kwa kinamama 3,725 na imefanikiwa kutoa huduma kwa wagonjwa wote 60,445.

Hospitali hiyo mpya yenye vifaa vya kisasa imejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 5.5. Ni mkopo wa IMF. Vifaa tiba vimegharimu Sh. milioni 682 na inaendeshwa kwa ushirikiano na sekta binafsi ambazo ni taasisi ya Saifee na Lancet kutoka India na ilianza kutoa huduma Mei mwaka huu.


**UNITED NATION CHILDREN'S FUND (UNICEF), UBALOZI WA SWEDEN NA WATAALAM MBALIMBALI DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na UNICEF, Ubalozi wa Sweden, na Wataalam mbalimbali watauza kwa mnada wa hadhara Magari, Generator na Wheel Loader tarehe 28 Okitoba, 2023 Jumamosi kuanzia saa 5:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Mnada utaanza Saa 5:00 asubuhi**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Toyota Land Cruiser Hard top | 1HZ Diesel Engine | 2016 | Bado |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon Y61 | ZD30 Diesel Engine | 2014 | Bado |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon Y61 | TB48 Petrol Engine | 2012 | Bado |
| 1 | Toyota Rav4 Station Wagon | 1AZ Petrol Engine | 2004 | Umelipwa |
| 1 | Generator 160 KVA 3 Phase | Perkins Diesel Engine | 2015 | Umelipwa |
| 1 | Generator 5.5 KVA | Diesel Engine Silence | - | Bado |
| 3 | Generator 6KVA, 3.2KVA & 3KVA | Petrol Engine | - | Umelipwa |
| 1 | Komatsu Wheel Loader | W100 Diesel Engine | 1984 | Umelipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza, Lion Street kuanzia tarehe 25 mpaka 27 Okitoba 2023, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 3 November, 2023 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

# CCM yasimamisha viongozi tuhuma kukihujumu chama

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Rukwa kimewasimamisha uongozi viongozi wa chama hicho wanaotuhumiwa kukihujumu kwa kuwauzia kadi za kielektroniki viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ili wazitumie katika mikakati yao ya kisiasa.

Akitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki jana, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Godfrey Mwanisawa, alisema viongozi hao walikuwa wakichukua kadi za wanachama na kumuuzia Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Rukwa, Sadrick Malila, maarufu kwa jina la Ikuwo ili atangaze kuwa wanachama hao wamehamia CHADEMA na wamerudisha kadi za CCM.

Alisema baadhi ya kadi hizo ni ya aliyekuwa mwana CCM mkongwe marehemu Chrisant Mzindakaya pia marehemu Zuberi Kauzeni ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi tawi la King'ombe Kata ya Majengo pamoja na kadi za wanachama waliohama mkoani Rukwa.

Alisema kuwa baadhi ya viongozi wa CCM waliokuwa wakiuza kadi hizo ni Chriss Mwalwanda ambaye ni Katibu Kata ya Majengo, Alexander Kasongo Katibu wa Siasa na Uenezi Kata ya Majengo na Paul Kawambula Katibu wa UVCCM Kata ya Majengo ambao wamesimamishwa ili kupisha uchunguzi wa tuhuma hizo.

"Oktoba 2, Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Rukwa aliita vyombo vya habari na kuonesha kadi za kielektroniki za wanachama wa CCM akidai kuwa wamerudisha na kujiunga na CHADEMA, kumbe baadhi yao walikuwa ni marehemu na wengine wamehama mkoa ambazo aliuziwa na viongozi hao wanaotuhumiwa," alisema Mwanisawa.

Alisema, kitendo alichofanya Mwenyekiti wa Chadema si sawa kwa kuwa mwanachama anayetakiwa kurudisha kadi anapaswa akabidhi yeye mwenyewe katika ofisi ya chama anachohamia ama katika mkutano wa hadhara wa chama, lakini kilichofanyika ni siasa chafu zisizo na tija katika nyakati hizi ambazo wanachama wanauelewa mkubwa wa masuala ya kisiasa.

Pia kutokana na maendeleo makubwa yaliyofanywa na serikali ya CCM hakuna mwanachama atayerudisha kadi yake kizembe na kuwataka wanachama wa chama hicho Mkoa wa Rukwa kutulia, kushikamana na kuwa na umoja kwa kuwa CCM ipo imara na haitatetereka kwa propaganda hizo chafu.

Katibu wa CCM Wilaya ya Sumbawanga, Tabu Hussein, alisema kwa kawaida kadi za wanachama baada ya kutengeneza ngazi ya taifa zinatumwa kwa viongozi wa mkoa, nao wanazipeleka ngazi ya wilaya na huzikabidhi kwa viongozi wa kata ambao walaiokuwa wakimuuzia kiongozi huyo wa Chadema.

Alisema tayari chama hicho kimeanzisha uchunguzi kwa viongozi hao wasio waadilifu pia kitachukua hatua kupitia wanasheria wa chama kwa mwanasiasa huyo wa upinzania aliyekuwa akifanya siasa chafu na kamwe CCM wilaya haitavumilia kuona wanasiasa wakiharibu nia yake nzuri ya kushinda chaguzi zijazo.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bagamoyo, Shauri Selenda, akimwagilia mti wa matunda alioupanda katika eneo la Shule ya Msingi Kimele iliyopo Bagamoyo mkoani Pwani katika kampeni inayoendeshwa na Benki ya Standard Chartered ya kupanda miti katika wilaya hiyo. Kulia ni Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Sarah Luwumba na wa pili kulia ni Mkuu wa Teknolojia na Operesheni wa benki hiyo, Christopher Vuhahula. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wazazi watakiwa kubadili mfumo malezi ya watoto

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Bagamoyo, Abubakari Mlawa, amesema wazazi wa wilaya hiyo wanatakiwa kubadili mfumo wa malezi ili kuwa na watoto wenye maadili na kupunguza vitendo vya ukatili.

Mlawa alisema wazazi pia wanatakiwa kuacha vitendo vya ukatili kwa watoto wao na kuwalea katika maadili yanayotakiwa kwa kuzingatia tamaduni za Watanzania.

"Wilaya ya Bagamoyo inaongoza kwa vitendo vya unyanyasaji kwa watoto wa kike, wapo wazazi wa kiume wanalala na watoto wao kesi nyingi zimeenda mahakamani, tunaendelea kusisitiza mabadiliko ya malezi kukomesha vitendo hivi," alisema.

Aliyasema hayo alipokuwa akihutubia mahafali ya 32 ya kidato cha nne Shule ya Sekondari Lugoba, Halmashauri ya Chalinze.

Kadhalika, Mlawa alisema wazazi wengi wa wilaya hiyo sio wafuatiliaji wa maendeleo ya watoto wao wanatoa kipaumbele kuandaa sherehe wanapohitimu.

Alisema wazazi wanatakiwa kuwasimamia watoto wao wasome kwa bidii ili wapate ajira kwenye viwanda vinavyojengwa katika wilaya hiyo badala ya kuacha nafasi hizo kuchukuliwa na wanaotoka nje ya wilaya na mkoa huo.

Mlawa ambaye ni Ofisa Habari wa Kampuni ya Subash Patel ambayo ni mlezi wa Shule ya Sekondari Lugoba, alisema wanatarajia kuanza utaratibu wa ujenzi wa uzio wa shule hiyo kudhibiti utoro.

Mkuu wa shule ya Lugoba, Abdallah Sakasa, aliwataka wazazi kuzingatia taratibu za shule na kutoruhusu kupokea watoto wao bila taarifa kutoka shuleni.

Kutokuwa na uzio katika shule hiyo na wanafunzi wengi kutoka maeneo ya karibu imechangia kuwa watoro kuondoka muda wanaotaka kurudi nyumbani huku wazazi wao wakishindwa kutoa taarifa baada ya kuwapokea.

Sakasa alisema kitendo hicho ni kero na kuomba kujengewa uzio utakaosaidia kuimarisha ulinzi kwa wanafunzi watakaotoa utaratibu maalumu.

Pia Sakasa alisema kuna uhaba wa vifaa vya maabara kwa ajili ya elimu ya vitendo kwenye masomo ya sayansi, maktaba pamoja na mabweni.

Aliishukuru serikali kwa kuendelea kuidhinisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo na vikimamilika hakutakuwa na uhaba kwenye eneo hilo.

# Wanafunzi wa kike wenye ulemavu waaswa

**Na Sabato Kasika**

KATIBU Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Abeida Rashid Abdallah, amewataka wanafunzi wakike wenye ulemavu kuchukulia hali hiyo kama ya kawaida na kusoma kwa bidii ili watimize ndoto walizojiwekea.

Abeida, alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi wakati akizindua vyoo rafiki vya wanafunzi wa kike wenye ulemavu, katika Shule ya Sekondari ya Jangwani.

Alisema, anajua vikwazo vyao lakini akawataka wasikate tamaa kutafuta elimu, na vikwazo hivyo viwe fursa ya kuwafanya waongeze bidii ili wawe viongozi wa baadaye.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinazungumza masuala ya watu wenye ulemavu kwenye vyombo vya maamuzi ili wasiachwe nyuma," alisema Abeida.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotekeleza miongozo mbalimbali ikiwamo wa masuala ya watu wenye ulemavu ilioitaja kwa jina la "Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Watu wenye Ulemavu".

"Lakini pia kuna sheria ya Tanzania Bara ya mwaka 2010 na kwa upande wa Zanzibar kuna sheria namba 9 ya mwaka 2006 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka jana, sheria zote hizo zinazungumzia wajibu wa utambuzi wa haki kwa watu wenye ulemavu, usawa na kutobaguliwa, kukuza uelewa," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa walimu wote katika shule mbalimbali nchini kuweka vyoo rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu, na sio vyoo tu hata njia ili mazingira nayo yawe rafiki.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Maisha ya Amani kwa Watu Wenye Ulemavu, iliojenga vyoo hivyo, Sofia Mbeyela, alisema ujenzi wa mradi wa vyoo rafiki kwa wasichana wenye ulemavu ulianza Julai, mwaka jana.

"Ujenzi huu umegharibu Sh. milioni 20,000 kwa vyoo vinne na chumba kimoja kwa ajili ya walengwa kubadili nguo wakati wakiwa katika siku zao za hedhi," alisema Sophia.

Alifafanua kuwa mradi huo utaendelea katika shule zote, huku akiwaomba wananchi, viongozi, mashirika binafsi na serikali kuendelea kuchangia ili kuwaondolea vikwazo wanafunzi wenye ulemavu.

Alisema anafahamu vikwazo vinavyowakabili wanafunzi wenye ulemavu na taasisi yake itaendelea kupambana ili wasiachwe nyuma kama sheria na miongozo ilivyoelekeza.

"Niwashukuru wadau wote waliojitolea kwa hali na mali kuchangia ujenzi huu, kwani awali shule ilikuwa na vyoo rafiki vitatu huku wanafunzi wakiwa 110, hali ambayo ilionyesha havitoshi," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Zulfa Swaleh wa kidato cha kwanza katika Sekondari ya Jangwani, alisema wamefarijika kupata vyoo hivyo na kuwaomba wadau kuwasaidia madaftari na vitabu kwa kuwa wengi wao wanatoka katika familia zenye kipato kidogo.





## World Vision yawanoa vijana

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

SHIRIKA la World Vision Tanzania, limeanza kuwapa mbinu vijana kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kupanda miti ili kupunguza athari za mazingira.

Akizungumza wakati wa kufunga mradi wa SAUTI YA VIJANA unaotekelezwa na shirika hilo kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU), Kamishna kwa Uhifadhi na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Profesa Dos Santos Silayo, alisema Dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi kwa kuleta matokeo mabaya na athari zake kuwakabili vijana kwa muda mrefu.

" Kundi la vijana tulilonalo lina miaka mingi ya kuishi, hivyo limekuwa linakabiliwa na changamoto ya kukumbana na mabadiliko ya tabianchi kwa muda mrefu wakipewa elimu ya kutunza mazingira wataweza kufanikisha jambo hilo," alisema Profesa Dos Santos.

Mkurugenzi wa World Vision Tanzania, James Andit, alisema mradi huo umewalenga vijana wajishughulishe na utunzaji wa mazingira kwa kuwa wathirika zaidi ni watoto kwa kukosa mahitaji ya msingi, ikiwemo chakula.

"Tunavyofunga mradi huu wa miaka mitatu tunajiandaa na mradi mwingine tutakao uzindua Desemba mwaka huu ujulikanao kwa jina la Ardhi ambao umelenga kuendeleza suala la mazingira," alisema.

Mratibu wa mradi huo, Shukrani Dickson, alisema kwa kipindi cha miaka mitatu wameendesha kampeni ya kitaifa ya upandaji miti kila wilaya ikiwemo ya matunda ili kuongeza lishe katika jamii.

"Tulikuwa na kampeni ya upandaji miti ambayo ililenga kupanda miti angalau miwili ya matunda kwenye kila miti mitano hivyo tunaamini kaya za jamii hizo zimeimarika," alisema Shukrani.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Saitoti Zelothe, alisema mradi huo umetekelezwa vizuri na kuahidi kuuendeleza utakapofikia kikomo kwa vile suala la mazingira si la kusubiri mradi mingine.

Mnufaika wa mradi huo, Christina Fundi, alisema hakuwa anaelewa kama mazingira yameathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi zaidi ya kushuhudia ukame.

Mradi huo ambao pia umetekelezwa katika wilaya za Korogwe na Handeni, umewawezesha vijana kuzalisha mazao yatokanayo na misitu ikiwamo asali na kilimo kinachozingatia uhifadhi wa mazingira.

# Tanzania yatajwa kinara usawa wa kijinsia

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi za Afrika inayoongoza kufuata na kuzingatia Itifaki ya Maputo (Maputo Protocal) ikiwamo kutambua umuhimu wa usawa wa kijinsia

Hayo yalisemwa jana na Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot wakati wa mkutano wa wadau wa taasisi na Azaki zinazojihusisha na masuala ya demokrasia na kutetea haki za binadamu nchini uliofanyika jijini hapa.

"Nchi za Tanzania na Uswisi zimekuwa mstari wa mbele kufuata na kuzingatia itifaki ya Maputo kwa kuwa zinatoa fursa sawa kwa wanawake na tumeona wanafanya kazi vizuri na kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa," alisema.

Balozi Chassot, alisema kutokana na itifaki hiyo haki za wanawake zimepatikana kutokana na kuwapo kwa mwamko mkubwa wa kutambua usawa wa kijinsia katika nchi hizo wanapewa fursa za uongozi.

Mkurugenzi wa Kituo cha Demokrasia na Haki za Binadamu cha Afrika, Hannah Forster, alisema kwa mujibu wa itifaki ya Maputo, kunahitajika kuendeleza usawa wa kijinsia kama ilivyothibitishwa katika sheria za Umoja wa Afrika (AU) na ushirikiano mpya wa maendeleo ya Afrika.

Alisema itifaki hiyo imetaja haki za wanawake na madhila wanayokutana nayo katika nchi zao, hivyo kuna umuhimu nchi 45 za AU ambazo zimeridhia makubaliano hayo kuzingatia na kusimamia kwa uhakika.

Alisema wanawake wana wajibu wa wa kulinda maadili ya Kiafrika kulingana na kanuni za usawa, amani, uhuru, heshima, haki, umoja na demokrasia.

Alisema, maazimio yanayohusiana, makubaliano, uamuzi, maagano na vyombo vingine na maeneo madogo yamelenga kuondoa kila aina ya ubaguzi na kuendeleza usawa kati ya wanawake na wanaume.

Rais wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, Nestor Kayobera, alisema kuna wasiwasi kuhusu sheria za kimataifa za haki ya binadamu na nchi wanachama kuondoa kila aina ya ubaguzi na vitendo hatari kwa wanawake kwa kuwa wengi wanaendelea kuwa waathiriwa wa vitendo hivyo.

"Kitendo chochote ambacho kinahatarisha kukua kwa kawaida na kinaathiri kuendelea kimawazo na kimwili kwa wanawake na wasichana kinafaa kukashfiwa na kuondolewa tujitahidi kuhakikisha haki za wanawake zinakuzwa, zinajulikana na kulindwa," alisema.



Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Tanga, ASF Leonard Mponeza (wa pili kushoto), akitoa elimu ya ukaguzi wa kinga na tahadhari za majanga ya moto kwa wafanyabiashara wilayani Muheza sambamba na kulipia tozo za ukaguzi na cheti cha usalama wa moto katika kikao kilichofanyika juzi. Kushoto ni Ofisa Habari wa jeshi hilo, Coplo Sharifu Salehe. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Teknolojia kubadili mifumo katika jamii kujadiliwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ASASI za Kiraia (AZAKI) zinatarajia kukutana na watendaji wa serikali, wananchi, wanazuoni na sekta binafsi jijini hapa kujadili maendeleo ya taifa kiteknolojia yanavyobadilisha mifumo katika jamii.

Mkurugenzi Mkazi wa CBM ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Wiki ya AZAKI kwa mwaka huu, Nesia Mahenge, alisema majadiliano hayo yatatoa fursa ya kuchangamana na wadau wa maendeleo kuangalia jamii ilipotoka na ilipofikia.

Mahenge, alisema kaulimbiu ya wiki hiyo ni 'Teknolojia na Jamii' na kwamba mjadala mkubwa itakuwa ni kujitathmini kwa kiasi gani wameweza kutumia teknolojia katika miradi na kazi zao na kuangalia maeneo waliyojifunza na yenye changamoto.

Alilitaja lengo kuu la wiki hiyo kuwa ni kuimarisha ushirikiano baina ya wadau wa maendeleo kati ya sekta binafsi, serikali na wananchi.

Alisema mijadala itakayojadiliwa imejikita zaidi katika ujumuishwaji wa teknolojia kwenye kazi za AZAKI, kuziwezesha na kuzipa nguvu jamii zilizotengwa, utetezi na ushirikiano uchechemuzi wa kidijitali.

"Pia tutajadili mchango wa teknolojia katika kuboresha elimu, utetezi wa jamii, ushirikiano, uwazi, ujasiriamali na maendeleo endelevu, kuimarisha usalama mtandaoni na hatua za kulinda takwimu au data za siri kwa mawasiliano salama," alisema Mahenge.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema mijadala hiyo itajikita katika masuala ya maadili kupokea matumizi ya maarifa bandia ili kuhakikisha maarifa hayo yanalenga kukabiliana na changamoto za kijamii na kuleta manufaa kwa jamii.

Mwakilishi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Deogratius Temba, alisema katika kuhakikisha kauli mbiu inakuwa jumuishi kwa jamii, watahakikisha makundi yaishio pembezoni hususani wanawake wanafikiwa.

## Mongela awa mbogo fedha za miradi, mapato

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha kuhakikisha fedha zinazotengwa zinakamilisha ujenzi wa miradi ya maendeleo.

Aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya kikazi katika halmashauri hiyo kukagua ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Sekei, majengo ya wagonjwa wa nje ya Hospitali ya Wilaya ya Arusha na Kituo cha Afya Levolosi.

Mongela, alisema ametoa kauli hiyo baada ya kubaini kuwa kumekuwapo na kasumba ya fedha za ujenzi wa miradi kwisha kabla ya mradi kukamilika na kuandaliwa mchakato wa kuomba nyingine za kukamilisha.


Vilevile, alikagua ujenzi wa vyumba vinane vya madarasa na matundu 22 ya vyoo katika shule ya Korongoni iliyopo Kata ya Lemara na vyumba 15 vya madarasa na matundu 21 ya vyoo vya Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Arusha.

"Mkurugenzi wa Jiji nakuagiza kuhakikisha fedha zinazotolewa na Serikali kujenga miradi hii zisije kuisha kabla miradi haijakamilika kwa kuwa jambo hilo halikubaliki hata kidogo," alisema na kuongeza kuwa:

"Kwa kuwa Serikali imetimiza wajibu wake wa kutoa fedha nyingi za kutekeleza miradi hii, sisi kama watumishi wa umma tunapaswa kubadili mienendo yetu ya utendaji kazi."

Katika hatua nyingine, Mongela, alieleza kusikitishwa na kitendo cha Halmashauri ya Jiji la Arusha kusuasua kukusanya mapato na kufikia asilimia 25 kwa robo ya kwanza ya mwaka wa bajeti.

"Suala kushuka kwa ukusanyaji wa mapato kwenye robo ya kwanza ya mwaka wa bajeti limenisikitisha na halijanifurahisha ndio maana nimewaandikia barua Mkurugenzi wa Jiji na Mkuu wa Wilaya," alisema.



# Burian awataka wananchi kuchangamkia hadhi Jiji

**Na Benny Kingson,**
TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Burian amewataka wananchi mkoani hapa kujiimarisha kiuchumi na kufanikisha mchakato wa Manispaa ya Tabora kupandishwa na kuwa na hadhi ya Jiji.

Balozi Burian alitoa rai hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelezea mikakati ya mkoa kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa ziarani mkoani hapa ikiwa ni pamoja na manispaa hiyo kupandishwa hadhi na kuwa Jiji.

Alisema, pamoja na kwamba kuna uhitaji wa vitu muhimu vya kukamilisha mchakato wa Tabora kuwa Jiji, dalili zinaashiria uwezekano wa kutangazwa endapo watafikia vigezo.

"Kuna mambo muhimu kama idadi ya watu, ukubwa wa eneo na mambo mengine tukiyakamilisha tutapitishwa kuwa Jiji, hivyo jiandaeni na wekeni mikakati ya kukuza biashara," alisema.

Alitaja fursa nyingine ambazo wanatakiwa kuchangamkia kuwa ni kwa kila mwananchi kufuga nyuki na kuuza mazao yatokanayo na wadudu hao.

Buriani alisema Tabora ina mizinga 800,000 ya nyuki na kuwataka kuendeleza uwekezaji katika mradi huo ili kuongeza uzalishaji asali na kuongeza pato la mkoa.

Aliwataka wananchi kuchangamkia mafunzo ya wiki mbili ya ufugaji nyuki yanayotolewa Chuo cha Nyuki ya jinsi ya kutengeneza bidhaa zinazotokana na mazao ya wadudu hao.

"Rais ameahidi kutusaidia kupata kiwanda cha kati cha kuchakata mazao ya nyuki hii ni faida kwetu na itatupa tija kubwa na kuongeza fursa katika mkoa wetu hivyo tukae mkao wa kula," alisema.

Aliwahimiza wawekezaji kuendelea kuwasili mkoani hapa kuwekeza hususani kwenye mazao yatokanayo na asali kwa kuwa yana soko kubwa ndani na nje ya nchi.

"Asali ya Tabora ina ubora wa hali ya juu na viwango vya kimataifa katika Soko la Dunia na ndani ya nchi," alisema.

**Alisema, pamoja na kwamba kuna uhitaji wa vitu muhimu vya kukamilisha mchakato wa Tabora kuwa Jiji, dalili zinaashiria uwezekano wa kutangazwa endapo watafikia vigezo.**

# Wakulima wasusa kilimo cha mpunga Kishapu

**Na Marco Maduhu,**
KISHAPU

WAKULIMA wa mpunga wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, wameachana na kilimo hicho kutokana na ukame uliosababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Baadhi ya wakulima hao walisema wameamua kuachana na kilimo hicho kutokana na kuendelea kupata hasara baada ya mazao yao kunyauka kwa kukosa maji.

Walisema wamekuwa wakiwekeza fedha nyingi katika kilimo hicho, baada ya muda mvua kuacha kunyesha mpunga umekauka na mwingine kudumaa kwa kukosa mvua za kutosha.

Mkulima wa Kijiji cha Mihama Kata ya Lagana, Mihambo Njile, alisema kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika kwani kitawawezesha kuvuna mpunga wa kutosha badala ya kutegemea kunyesha kwa mvua.

"Wananchi wengi katika wilaya hii ya Kishapu tuliachana na kilimo cha mpunga sababu ya ukame, kwasababu kuna mradi wa kilimo cha umwagiliaji, mifereji iliyojengwa maji ya kwenye mito yatakuwa yakiingia mashambani mwetu moja kwa moja na kuwa na maji mengi," alisema Mihambo.

Kabea Joseph, Mkulima wa Kijiji cha Mwajiginya, aliishukuru Serikali kwa kutekeleza mradi wa umwagiliaji kijijini humo akisema utaongeza uzalishaji wa mpunga na kupata mchele wa kutosha.

Mtendaji wa Kijiji cha Mihama, David Joseph, alisema wakulima walisusa mashamba yao kutokana na ukame na kukosa maji ya kutosha kwenye majaruba.

Ofisa Umwagiliaji wa Halmashauri ya Kishapu, Mwinula Ntwangi, alisema vijiji 22 vimewekwa katika mkakati wa kupatiwa mradi wa umwagiliaji ili kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua kwa kipindi cha mwaka mzima.

Ntwangi, alisema Serikali imetoa fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kilimo cha umwagiliaji na kuacha kutegemea mvua.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Sabinus Chaula ambaye pia ni Ofisa Kilimo Mifugo na Uvuvi, alisema Serikali imetoa fedha na kuanza kutekeleza miradi ya kilimo cha umwagiliaji kwa vijiji 22 wilayani hapa.

Alisema mpaka sasa wametekeleza miradi ya umwagiliaji katika vijiji saba kwa kujenga mirefeji, ambayo itakuwa ikitoa maji kwenye mito na kupeleka kwenye mashamba ya mpunga na mazao mengine.

Alisema, pia wamewekeza kwenye ujenzi wa malambo ya maji ambayo yatatumika katika kilimo hicho na kunyweshea mifugo.

Alisema katika Kijiji cha Beledi wamejenga lambo la maji kwa Shilingi milioni 260, Mugunda Shilingi milioni 15, Kiloleli Shilingi milioni 300 na Kijiji cha Mihama Shilingi milioni 125.




Polisi wa Kikosi Maalumu cha Kupambana na Dawa za Kulevya Tarime, Rorya, mkoani Mara, akiangalia gunia za bangi na pikipiki saba zilizokamatwa katika operesheni maalumu ikiongozwa na SP Mihayo. **PICHA: SAMSON CHACHA**

# Barabara kikwazo utoaji bima milimani

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MAWAKALA wa huduma za bima wamesema ukosefu wa barabara ni kikwazo cha utoaji wa bima za majanga ya moto kwa wananchi waishio maeneo ya milimani baada ya nyumba zao kuteketea.

Kauli hiyo imetolewa jijini hapa na mawakala wa huduma za bima wakati wa semina ya kuwakumbusha namna ya kuendelea kubuni mbinu za kuboresha huduma zao katika jamii iliyoandaliwa na Kampuni ya Jubilee Allianz General Insurance.

Akizungumza kwa niaba ya mawakala wenzake, Person Mlote kutoka Twilumba Insurance Agent, aliiomba Serikali kuangalia namna ya kutengeneza miundombinu ya barabara kwa wananchi waishio milimani ili kujikinga na majanga ya moto.

"Wananchi wamekuwa wakipata hasara kubwa nyumba zao zinapo ungua na hii ni kutokana na miundombinu isiyo rafiki inayosabisha gari la zimamoto kushindwa kufika maeneo husika," alisema.

Alisema majanga ya moto yanapotokea milimani ni vigumu kwa kampuni za bima kuwapatia bima za moto wananchi waishio huko kwa kuogopa hasara, itokanayo na kuwalipa fidia kubwa baada ya nyumba zao kuteketea bila ya kupata msaada.

Meneja Mawakala wa Jubilee Allianz General Insurance, Mary Ndege, aliwataka vijana wenye taaluma ya bima kuhakikisha wanatafuta fursa za kujiajiri kuliko kusubiri ajira za serikali na kampuni.

Katika semina hiyo, Jubilee ilitoa zawadi za kompyuta, televisheni na vyeti kwa mawakala waliofanya vizuri.

Mshindi wa kwanza, Justine Mjema, aliyepatiwa zawadi ya kompyuta na televisheni, aliwataka vijana kuongeza bidii katika kazi zao ikiwa ni pamoja na kujiunga na utoaji wa huduma za bima katika jamii kama mawakala.

**"Wananchi wamekuwa wakipata hasara kubwa nyumba zao zinapo ungua na hii ni kutokana na miundombinu isiyo rafiki inayosabisha gari la zimamoto kushindwa kufika maeneo husika," alisema.**



Ukurasa 12

**VITA VS UKEKETAJI**

Mdau ataka Afrika iingize athari kwenye mitaala


Ukurasa 13

TEHAMA ilivyojenga sekondari watoto 800, ushuhuda bosi UWT


Nipashe

# TESA

Jumanne Oktoba 24, 2023

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Taarifa za maangamizo ya watoto zilivyoamsha makanisa kuwanusuru**

ELIMU

NA SAID SINDO, GEITA

# Shule 'isiyo na walimu' inavyofanya maajabu

• Ni kivutio wazazi, watoto kuikimbilia

SEKONDARI ya Lutozo inayopatikana katika mamlaka ya mji mdogo Katoro mkoani Geita, imekuwa ni kivutio kwa jinsi ambavyo licha ya kukabiliwa na changamoto lukuki, inafanya maajabu kitaaluma.

Ajabu ya kwanzani ni kwamba Lutozo ina walimu wawili wa bailojia ambao hufundisha wanafunzi 2,049 wa mikondo 26 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, lakini inatisha kwenye somo hilo kwenye ufaulu.

Shule hiyo ya kata ya Katoro inafanya vizuri katika mitihani ya taifa kwa miaka mitano mfululizo na tena kwa 2022 ilikuwa ya kwanza kiwilaya kwa kupata daraja la kwanza, la pili na la tatu kwenye mitihani ya kidato cha pili na cha nne.

Mwalimu wa Taaluma wa shule hiyo, Ladislaus Mukama, anasema kwa mwaka jana wanafunzi 256 wa kidato cha nne waliofanya mtahani, walifaulu kwa wastani wa asilimia 57 kwa kuanzia daraja la kwanza, lapili na la tatu isipokuwa mmoja pekee aliyepata sifuri.

"Kwa matokeo haya tulivuka malengo ya mkoa, maana mkoa ulikusudia kwamba shule zote zifaulu katika daraja la kwanza, la pili na la tatu kwa asilimia 45 -50, kwa hiyo sisi tukavuka lengo kwa asilimia 57," anasema mwalimu Mukama

Aidha, anataja nidhamu kuwa ndiyo imekuwa msingi mkubwa na dira ya mafanikio kwa kuzingatia kauli mbiu ya shule hiyo inayosema."Nidhamu na taaluma'.

"Tuna nidhamu. Kwasababu



Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Lutozo iliyoko Katoro mkoani Geita, akiwa darasani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

eneo la Katoro iliyopo shule hii ni kitovu cha biashara na shughuli nyingi za kiuchumi zakiwamo madini, hivyo kuwa rahisi wanafunzi kushawishika na kupotoshwa."

"Inatubidi sasa mimi na mwenzangu tufundishe vipindi utakavyoweza kuvimudu, mpaka unakosa muda wa kupumzika. Lakini, kwasababu tumejipambanua kufanya kazi, tunaona si shida, tunapambana kufanya hivyo. Kwahiyo serikali pia, iendelee kuajiri walimu wa sayansi hasa katika shule hizi zinazofanya vizuri," anaongeza.

Walimu katika shule hiyo hutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilomita tano kutokana na shule kujengwa pembezoni mwa mji ambako gharama ya kukodi gari, pikipiki au bajaji hufikia hadi Shilingi 3,000.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wanafunzi wanasema licha ya shule hiyo kufanya vizuri wanakabiliwa na changamoto ya kutembea umbali mrefu, ukosefu wa miundombinu, maji na ukosefu wa bweni kwa wasichana hali inayohatarisha usalama wao kutokana na uwepo wa vishawishi vingi.

"Tunachangamoto ya maji, hasa kipindi cha kiangazi, kuna kisima ambacho hukauka, kwahiyo tunalazimika kutoka na maji nyumbani ili kukidhi mahitaji ya msingi ya usafi kama kwenye vyoo, madarasa na jikoni. Anaeleza mmoja wao.

Wanaeleza kuwa wana vyumba vitatu vya maabara, lakini kimoja ndicho kinachotumika hali inayosababisha masomo yote matatu (fizikia, kemia na bailojia) kufanyika kwenye chumba kimoja cha maabara kwa kusubiriana wakihusika wanafunzi wote kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Pamoja na kwamba changamoto wanazokutana nazo walimu na wanafunzi zinafanana kwa kiasi kikubwa, watoto hao wanakabiliwa na matatizo mengi zaidi, ambayo ikiwa yatatuliwa mapema, yatakuza ubora wa elimu katika shule hiyo, wanaeleza.

Mwalimu Mkuu, Revocatus Maraha, anasema amekuwa akipokea simu kutoka Dar es salaam, Mbeya, Arusha na maeneo mengine wazazi na walezi wakiulizia nafasi za kuhamia huku wengine wakihoji kama shule hiyo ni ya bweni.

"Unapigiwa na mzazi au mlezi anakuuliza kama atapata nafasi ya kuhamia, unamwambia nafasi zimejaa, ukimkatalia anapiga kwa mkurugenzi inabidi kutii maelekezo."

Anaongeza kuwa:"Kipindi cha nyuma tulikuwa na uhaba wa madarasa, kutokana na ufaulu mzuri wa kitaaluma, serikali imetuwezesha madarasa mawili kupitia Mradi wa Programu ya Kutekeleza Elimu kwa Matokeo (EP4R),vilevile imetujengea vyumba 12 vya madarasa, kwakweli kwa sasa hali ni nzuri," anasema Maraha.

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA SABATO KASIKA

VITA VS UKEKETAJI

# Mdau ataka Afrika iingize athari kwenye mitaala




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Riziki Pembe, akizungumza kwenye jukwaa la kupinga ukeketaji. **PICHA: SABATO KASIKA**

MADHARA ya ukeketaji yamewakutanisha wadau wanaopambana na ukatili huo kutoka nchi 21 za Afrika kwa muda wa siku tatu jijini Dar es Salaam, wakiweka mipango ya kuukabili.

Katika mkutano wa kutokomeza ukeketaji Afrika, wadau hao wanatoa maoni mbalimbali ya kukabili ukatili huo, miongoni mwake ni kutaka nchi za Afrika kubadili mitaala ya elimu na kuingiza somo la ukeketaji, ili kuwasaidia watoto kufahamu madhara yake.

Huo ni mchango wa Sentamim Mussa kutoka Kenya ambaye anaamini kuwa watoto wakipata elimu ya madhara ya ukeketaji tangu wakiwa shuleni, itawasaidia kuepuka vitendo hivyo.

Anasema elimu ina nguvu kubwa ya kumpa mwanafunzi maarifa, mbinu na ujuzi na kwamba njia hiyo ya kubadili mitaala ya elimu na kuingiza somo la ukeketaji inaweza kusaidia kuokoa wasichana wengi.

"Wakati tukiendelea na vita dhidi ya ukeketaji katika nchi zetu, ninadhani kuna haja kwa nchi za Afrika kubadili mitaala ya elimu ili kuwasaidia kufahamu madhara ya ukeketaji," anasema Sentamim.

> Tunashirikiana kuimarisha utendaji kazi wa polisi, uhamiaji, maofisa ustawi wa jamii na maafisa maendeleo ya jamii katika kutoa elimu itakayosaidia kuondokana na vitendo hivyo.

Anasema, kila mmoja kwa nafasi yake ana wajibu wa kushiriki katika hiyo, na kwamba kukiwa na somo la ukeketaji kuanzia shule za awali, watoto watakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu madhara ukeketaji.

Katika mkutano huo wa pili wa kimataifa kuhusu kutokomeza ukeketaji, anasema utolewaji mapana wa elimu kuhusu madhara ya ukeketaji ni suluhisho la kutokomeza vitendo hivyo barani Afrika.

"Wito wangu ndio huo, nilishaufikisha kwa serikali ya nchi yangu na nimeona niutoe hapa wakati huu ambao tumekusanyika kutoka nchi mbalimbali za Afrika kwamba, serikali zetu ziangalie uwezekano wa kubadili mitaala ya elimu ya kuweka somo la ukeketaji," anasema.

#### HALI YA UKEKETAJI

Akifungua mkutano huo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anasema wanawake na wasichana zaidi milioni 200 duniani wamekeketwa.

Katika ufafanuzi wake anasema wanawake na wasichana zaidi ya milioni 20 kati ya hao, wamekeketwa kupitia watalaam wa afya, huku akiongeza Afrika inatakiwa kuunganisha nguvu kukomesha vitendo hivyo.

Waziri huyo wa Maendeleo ya Jamii, anaongeza kuwa, kwa sasa wanawake na wasichana zaidi ya milioni 68 duniani, wako katika hatari ya kukeketwa, huku bara la Afrika ikiwa kwenye hatari zaidi.

Aidha, anasema kwa sasa imenaza mikakati ya kupambana na vitendo vya ukeketaji vinavyovuka mipaka ambavyo vimekuwa vikisababisha vifo na athari za kiafya na kisaikojia kwa watoto wa kike.

Dk. Dorothy anasema baadhi ya wasichana wamekuwa wakivushwa kwenda nchi jirani au kutoka nchi jirani na kuingizwa nchini kukeketwa, pale wanahusika wanapoona katika nchi zao wamebanwa.

"Tunashirikiana kuimarisha utendaji kazi wa polisi, uhamiaji, maofisa ustawi wa jamii na maafisa maendeleo ya jamii katika kutoa elimu itakayosaidia kuondokana na vitendo hivyo," anasema Dk. Dorothy.

Anasema Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki zinazokabiliana na vitendo vya ukeketaji vinavyovuka mipaka na imejipanga kupambana navyo ili mipaka ya Tanzania na nchi nyingine iwe salama kwa watoto wa kike na kuondoka na vitendo vya ukeketaji.

Mkutano wa wadau hao unamalizika ukiwa na maazimio ya kutokomeza ukeketaji, miongoni mwake yalikuwa ni kushirikiana ili kubadili mitazamo ya jamii kuhusu ukeketaji.

Wadau hao pia wanaazimia kuunda ushirikiano wa kimkakati kuwa na vipindi katika mitandao vya kubadilishana uzoefu na kuimarisha uhusiano uliopo ili kukomesha mila potofu zenye madhara.

Vilevile, wadau hao wanaazimia kuendeleza juhudi za kuwalinda wanawake na wasichana dhidi ya makovu ya maisha na kisaikolojia yanayosababishwa na ukeketaji.

Aidha, wadau wanaazimia kujitolea kwa nguvu zote kuhakikisha vita dhidi ya ukeketaji inafanyika kwa kila nchi kuanzia ndani, kitaifa na kimataifa na kubadilishana taarifa.

#### TUTUMIE TEKNOLOJIA

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Riziki Pembe anatamani teknolojia itumike kuwakutanisha wadau hao ili kubadilishana mawazo na kutekeleza maazimio yao ili kutokomeza ukeketaji Afrika na duniani kwa ujumla.

Ni wakati wa kuhitimisha mkutano wa wadau hao, anasema hakuna sababu ya kuendelea kukiuka haki za binadamu na ukatili kwa wanawake na wasichana kutokana na mila zenye madhara.

"Mikakati madhubuti iliyowekwa katika maazimio ya mkutano huo yataleta mabadiliko kwa kizazi kijacho katika kupambana na ukeketaji. Teknolojia itumike kuwakutanisha, mbadilishane mawazo na kutekeleza maazimio mliojiwekea ili kutokomeza kabisa ukeketaji Afrika na duniani kwa ujumla," anasema Riziki.

Waziri huyo anawataka wadau hao kufikisha maazimio katika mamlaka ya nchi zao ili hatua ziweze kuchukuliwa katika kupambana na kutokomeza vitendo vya ukeketaji Afrika.

Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatma Toufiq anasema sheria ya kupinga ukeketaji ilitungwa mwaka 1998 na katika kuendeleza mapambano serikali imeandaa mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukeketaji na sheria ya mtoto.

TEKNOLOJIA
NA RESTUTA JAMES

# TEHAMA ilivyojenga sekondari watoto 800, ushuhuda bosi UWT

UVUMBUZI na mabadiliko ya kasi ya kiteknolojia yanayoendelea duniani yamebadili namna watu wanavyoishi huku yakirahisisha namna ya kufanya kazi, biashara, malipo na kupashana habari.

Yote hayo hufanyika ndani ya muda mfupi kufanikisha kupata taarifa za masoko, bidhaa na huduma zinazohitajika, kujifunza, kufundisha, kuuza, kununua na kulipa gharama mtandaoni.

Aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe na Korogwe ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Jokate Mwegelo, anatoa ushuhuda wa namna mitandao ya kijamii ilivyombeba.

Ilifanikisha malengo mbalimbali ikiwamo kampeni na harakati za kikazi , akiwa Kisarawe alitumia Instagram, akafanikisha kampeni ya kujenga sekondari ya wasichana kupitia kampeni ya 'tokomeza ziro'.

Anajivunia kujengwa sekondari ya bweni ya wasichana ambayo hivi sasa ina wanafunzi zaidi ya 800, ikijulikana kama Sekondari ya Wasichana ya Jokate Mwegelo.



Katibu Mkuu wa UWT, Jokate Mwegelo, (aliyesimama) akizungumza kwenye jukwaa la dijitali hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"Nimekutana na watu wengi ambao wamenishika mkono kwenye utumishi wangu, nimesema yale yanayofanywa na serikali na wananchi wameelewa, rai yangu kwa wanawake na wasichana ni kutumia mitandao ya kijamii kujisemea, kujitangaza na kutanua wigo wa mawasiliano," anasema Jokate katika kongamano la wanawake na soko la dijitali, lililofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

Anaongeza: "Wanawake na mabinti tujiamini, mitandao ya kijamii ina fursa nyingi na inatupa nafasi ya kwenda popote duniani bila pasi ya kusafiria wala visa unaingia nchi yoyote na kutoka bila kikwazo wala kizuizi."

Wachambuzi wa masuala ya teknolojia wanaeleza kuwa majukwaa ya kidijitali yana nguvu kutokana na uwezo wake wa kufikisha taarifa bidha kwa jamii kubwa ndani ya muda mfupi.

Katika muktadha wa hali ya sasa duniani, majukwaa ya kidijitali yamegawanyika katika biashara au huduma mtandao (e-commerce), malipo ya fedha na miundombinu ya kielektroniki yaani aplikesheni ambazo ndizo majukwaa yenyewe.

Mwanahabari na mjasiriamali, Carol Ndosi, ambaye ni miongoni mwa wanawake wanaohamasisha matumizi salama ya mtandao, anasema maendeleo ya kiteknolojia ni eneo ambalo linapaswa kumwingizia mtu kipato kama litatumiwa vizuri.

"Tunaweza kufanya mambo mengi ikiwamo kupata maarifa na fursa. Mitandao tunatumia, lakini je, ukiingia mtandaoni unafanya nini? Unaipa pesa au mitandao inakupa wewe pesa?" anahoji.

Swali hilo limemfanya Carol kuanzisha harakati za kumsaidia mwanamke kuzijua fursa za kiteknolojia na kidijitali, akianzisha miradi ya mafunzo na makongamano ya kuhamasisha matumizi ya tehama kwa wanawake.

Anasema mila, desturi na utamaduni ni mambo yanayokwaza ushiriki wa wanawake kwenye fursa za kidijitali akieleza kuwa amejitosa kuhakikisha wanawake hawabaki nyuma kunufaika.

Carol ambaye ni mwanzilishi wa jukwaa la The launch pad na Techno Woman, anasema ushiriki duni wa wanawake kwenye masuala ya dijitali, ulimlazimu kuanzisha harakati za ujumuishaji wa wanawake kwenye masuala ya kidijitali tangu mwaka 2018.

"Tumejikita katika kuwajengea uwezo na kuweka miundombinu ambayo inaweza kukabiliana na ukatili wa kijinsia mtandaoni miradi tunayoitekeleza ni pamoja na digital Tanzania ambayo inatoa mafunzo kwa wanawake pamoja na she take incubator ambayo inawaatamia wanawake wanaobuni na kuvumbua masuluhisho ya kidijitali (aplikesheni za simu)," anasema.

Carol anaongeza kuwa: "Tukaona tutengeneze jukwaa ambalo litawalea wavumbuzi wa kike ambao wataweza kuja na masuluhisho ya kidijitali."

Anasema harakati hizo zimeanza kuzaa matunda kwa kuwa wapo wanawake ambao wameanzisha aplikesheni na wengine wanatumia mitandao na majukwaa ya kidijitali kwa manufaa makubwa.

Mtaalamu wa lishe na mhamasishaji wa unyonyeshaji, Idda Katigula, anasema miaka mitano iliyopita alianza harakati za kusaidia wanawake wanaonyosha, mbinu za kutimiza jukumu hilo muhimu kupitia mtandao.

Anasema amefanikiwa kufundisha wanawake 2,500 na kwamba wengine 20,000 wameuliza maswali na kuwapa ufafanuzi uliowasaidia.

> "Tunaweza kufanya mambo mengi ikiwamo kupata maarifa na fursa. Mitandao tunatumia, lakini je, ukiingia mtandaoni unafanya nini? Unaipa pesa au mitandao inakupa wewe pesa?

"Nilipata changamoto nilipojifungua mtoto wangu wa kwanza ambaye hakuwa anapenda kunyonya hata baada ya kufanya jitihada nyingi kumsaidia. Iliniumiza na ilinifanya nihangaike sana kutafuta msaada hadi nilipokutana na daktari mmoja bingwa ambaye nilimweleza shida yangu akanisaidia na kumfanya mtoto akubali kunyonya niliona huenda kuna wanawake wengi wanapitia shida hii na ndipo nikaanza harakati za kuwaelimisha wengine," anasema Idda.

Anasema aliamua kutumia mitandao ya kijamii kwani aliona ni jukwaa ambalo lingewafikia watu wengi ndani ya muda mfupi na kwa muda mrefu.

"Niliende kusoma masuala ya lishe na sasa natengeneza vyakula vyenye virutubisho vinavyochochea maziwa ya mama anayenyonyesha. Nawafundisha pia mbinu za unyonyeshaji na kwa kweli naona watu wamelipokea vizuri. Lengo langu ni kufanikisha kuanzisha benki ya maziwa ya mama hapa nchini ili kuwasaidia watoto wanaozaliwa na mama kupata matatizo kiasi cha kushindwa kunyonyesha," anasema.

Mtengenezaji wa ice-cream, Mercy Kitomari, anasema amekuwa akitengeneza na kutangaza bidhaa yake mtandaoni ambako amepata wateja wa jumla na rejareja.

"Kwa miaka 10 sasa nimekuwa nikitengeneza na kuuza ice-cream mtandaoni na pia nimeanzisha mafunzo ya namna ya kutengeneza bidhaa hii huko huko mtandaoni, huwa natangaza darasa na gharama za mafunzo watu wanalipa naanza kuwafundisha," anasema.

Mercy anaongeza kuwa: "Ukitumia vizuri mitandao unaweza kutengeneza kipato kikubwa. Mimi nimefanikiwa na nina hakika mwingine anaweza kufanya kama mimi au hata kunizidi."

Moja ya jukwaa lililovumbuliwa na wanawake ni inayomwezesha mtumiaji kurekodi mapato na matumizi yake kila siku.

"Inakuwezesha kuishi ndani ya kipato chako kwa sababu baada ya kurekodi mapato na matumizi inaweza kukushauri matumizi yako ya fedha tumetengeneza mfumo wa akili bandia ya kukushauri matumizi yako," anasema Zubeda Mbonye, mwakilishi wa aplikesheni hiyo.

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Taarifa za maangamizo ya watoto zilivyoamsha makanisa kuwanusuru



Wanafunzi wakiimba katika uzinduzi wa kampeni ya 'Ulinzi na Usalama wa Mtoto' katika mji mdogo wa Ilula. **PICHA: EAGT**

WATOTO wenye umri wa kuwa darasani hawasomi. Wamekuwa waathirika wakubwa wa ukatili, vitendo hivyo vikiongezeka kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwenye mji mdogo wa Ilula ulioko wilayani Kilolo Mkoa wa Iringa.

Mateso hayo yawaamsha wadau mbalimbali wanaoandaa kampeni maalumu kuwalinda na kuwatunza watoto hao ili waishi salama, wakiwekeza kwenye kutoa elimu shule za msingi na sekondari kuhusu malezi, ulinzi wa mtoto, namna ya kuripoti masuala ya ukatili yanapotokea , hatua za kuchukua kukabiliana na ukatili, haki zao na matumizi sahihi ya mitandao na athari za ushoga na ulawiti.

Mratibu wa Kituo cha Maendeleo ya Mtoto na Kijana, cha Kanisa la Evangelist Assemblies of God Tanzania (EAGT) la mji mdogo wa Ilula, Bujo Paight, anasema ukiutembelea katika mji huo utashangaa jinsi watoto wanavyoumizwa na ubakaji, kutelekezwa, mimba za utotoni kuongezeka huku wengine wakitumbukizwa kwenye ushoga na ulawiti kwa kukosa malezi bora, uangalizi na usimamizi.

Akizungumza na Nipashe Paight, anasema baada ya kuona ukatili unaongezeka, makanisa matatu kutoka mji huo yamezindua kampeni maalumu ya kupinga ukatili kwa watoto inayojulikana kama ' Kampeni ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto' ili kutoa elimu kwa wazazi na walezi, watoto , walimu na jamii nyingine.

Lengo kuu la kampeni ni kuongeza uelewa juu ya umuhimu wa kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili, unyonyaji, ndoa za utotoni na mimba za utotoni na aina nyingine zote za ukatili ili kuhakikisha kwamba wale walio katika mazingira magumu/hatarishi zaidi katika jamii yetu hawapati ukatili na wanaishi katika mazingira salama,' anasema.

Makanisa ya Assemblies of God (EAGT), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Kanisa la Pentekoste Tanzania (KLPT) na kwamba kampeni hiyo imeandaliwa na vituo vya maendeleo ya mtoto na kijana vilivyo chini ya makanisa haya yanayofanya kazi ya kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwa kushirikiana na asasi ya Compassion International Tanzania (CIT) .

Anaongeza kuwa kampeni hiyo iliyozinduliwa na mbunge wa Kilolo, Justin Nyamoga mapema mwezi huu itafanyika kwa miezi mitatu, na kwamba hadi sasa makanisa haya yanawahudumia watoto na vijana zaidi ya 900 kiakili, kiafya, kiroho na kijamii .

"Tumegundua tatizo hili kutoka kwenye taarifa za baadhi ya watoto waliopata mafunzo wakati wa kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia Novemba mwaka jana waliofika kutoa taarifa ofisini kwetu kuhusu changamoto zinazowakabili watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na hatimaye sisi kwenda kufuatilia," anasema Paight,.

Aidha, kampeni itawaelimisha vijana, wanafunzi, walimu, wazazi, walezi, na jamii kwa kuwa wote wana wajibu wa ulinzi na usalama wa watoto akiongeza kuwa wanafunzi, wototo na vijana watafundishwa athari za usagaji na ushoga, malezi, haki zao, ulinzi wa mtoto, namna ya kuripoti masuala ya ukatili yanapotokea , hatua za kuchukua kukabiliana na ukatili, na matumizi sahihi ya mitandao na athari za ushoga na ulawiti.

"Tunataka kuwafundisha athari za usagaji na ushoga ili kusaidia watoto ambao hawajajiingiza kwenye vitendo hivi wasiingie na tunataka wawe wazazi na walezi bora wa kizazi kijacho," anasema Paight,.

Wakati wa kutoa elimu, wazazi na walimu watafundishwa malezi, ulinzi wa mtoto, aina za ukatili na namna ya kuripoti kunapotokea masuala ya ukatili na haki za watoto, anasema Paight.

"Tutatoa elimu kwa walimu mashuleni kwani tunaamini wao ni walezi lakini pia kwasababu ukatili mwingi wa kimwili umekuwa ukifanywa na wao aidha kwa kujua au kutokujua ," anasema Mratibu Paight.

Mbali na hilo, watatoa elimu kwa jamii nzima ya mji wa Ilula, kutoa elimu ya masuala ya ulinzi wa mtoto kwa makundi yanayoonekana kuwa hatarishi zaidi kwa usalama wa watoto ambayo ni madereva wawe wa bajaji, daladala na bodaboda, lakini mwisho ni kutoa elimu ya malezi kwa makundi yote.

Anasema, wanafanya hivyo si tu kwa kuwaelimisha watoto na vijana wetu kuhusu haki zao bali pia kwa kuwaelimisha watu wazima, wazazi, walezi, walimu na jamii ambao wana wajibu wa kuhakikisha ulinzi na usalama wa watoto.

Mbunge wa Kilolo, Justin Nyamoga, anashukuru viongozi wa dini, makanisa kwa kushirikiana na shirika la Compassion kuzindua kampeni ya ulinzi na usalama wa mtoto katika mji mdogo wa Ilula ili kuunga mkono juhudi za serikali kulinda mtoto.

Mkoa wa Iringa ni moja kati ya mikoa yenye kiwango kikubwa cha ukatili wa kijinsia, watoto wanabakwa, wazazi wanajinyonga kwa sababu ya kumbaka mtoto wake, ulawiti, kutelekezwa, kupigwa, kunyimwa elimu na ukatili dhidi ya wasichana.

"Kampeni hii ni muhimu ili kusaidia wazazi kupata elimu, natoa wito kwa watendaji wa kata, vijiji na vitongoji kuhakikisha kuwa katika mikutano yenu muandae mikutano maalumu ya wazazi wote kusikiliza kampeni hii ili watoto wapate malezi bora na kujenga kizazi bora."

Pia, viongozi wa dini watoe fursa kwenye ibada zao ili waumini wapate elimu hii, ujumbe huu ufikie waumini kwenye maeneo yao, anasema Nyamoga.

## Shule 'isiyo na walimu' inavyofanya maajabu

**INATOKA UK.11**

Kwa upande wa maji anasema wamekwisha wasiliana na diwani wa kata hiyo na kuahidi kulifuatilia huku akiongeza kuwa wasanifu maji tayari wameshapita kwenye shule hiyo na kwamba kabala ya mwaka kuisha watakuwa wametatua changamoto hiyo.

Chama cha Walimu (CWT) Mkoa wa Geita , wakati wakihitimisha sherehe za Mei Mosi mwaka huu 2023, kilimtunuku hati ya pongezi ya utumishi bora Mwalimu Mkuu wa Shule ya Lutozo, Maraha pamoja na mwalimu wa baiolojia Ladislaus Mkama kwa ufaulu mzuri katika somo hilo na kujitoa, utumishimzuri na ushirikiano alionao na walimu wenzake.

**NENO LA SERIKALI**

Mkurugenzi Mtandaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Rajabu Karia, anasema serikali inazifanyia kazi changamoto hizo na tayari mwaka huu ina mpango wa kuajiri walimu wa masomo ya sayansi na hisabati kwa shule za sekondari ambao wengi wataelekezwa katika shule za pembezoni.

"Hawa walimu safari hii hawatapelekwa kwenye halmashauri ili iwasambaze, bali watapangiwa moja kwa moja vituo vya kazi kutoka wizarani, lengo ni kupunguza uhaba katika shule zetu za mikoani. Tunazitaka halmashauri kuhakikisha zinagawanya walimu kutoka maeneo ambayo yana ziada na kupeleka sehemu zenye upungufu," anasema Karia.





# Serikali yazidi kubana mianya ya 'ulaji'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu, Nchemba amesema matumizi sahihi na salama ya mifumo ya kielektroniki serikalini ni suluhisho la kudumu kuziba mianya ya upotevu wa rasilimali ikiwamo mapato ya fedha kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

Dk. Nchemba alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita jijini hapa wakati akipokea na kuzindua Mfumo wa Kieletroni wa Kuratibu Ununuzi wa Mafuta Serikalini (GIMIS) kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene.

GIMIS umesanifiwa na kujengwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA).

Alisema matumizi ya mifumo imara ya kielektroniki yanasaidia kuondoa mianya ya upotevu wa rasilimali za Serikali na kudhibiti watumishi wasio waadilifu, kwa kuwa malipo yote yatalipwa kupitia njia sahihi na salama katika taasisi husika.

"Tukifanya kazi kupitia mifumo ya kielektroniki tunapunguza makosa mengi ya kibinadamu, hivyo matumizi sahihi ya mifumo hii yatatuwezesha kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wetu ikiwa ni pamoja na eneo la ukusanyaji wa mapato ya Serikali," alifafanua Dk.Mwigulu.

Akieleza kuhusu mfumo huo, alisema unatumiwa na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na kwamba majukumu yote yanatekelezwa kupitia mfumo huo kurahisisha na kuongeza ufanisi.

Waziri Simbachawene, alisema lengo la mfumo huo ni kurahisisha utendaji kazi wa GPSA katika uuzaji wa mafuta Serikalini, kuweka uwazi na kutunza kumbukumbu za matumizi ya mafuta katika kila taasisi ya umma.

Alisema zaidi ya taasisi nunuzi 7,070 zinatumia mfumo huo na taarifa za matumizi ya mafuta kwa kila taasisi zinatunzwa katika mfumo huo na kusaidia uandaaji, usimamizi wa mipango ya bajeti ya ofisi na udhibiti wa matumizi wa mafuta kwa taasisi za umma.

"Lengo la mfumo huu ni kuhakikisha matumizi sahihi ya mafuta kwa taasisi za umma na kuokoa fedha zilizokuwa zikipotea kutokana na kutokuwapo kwa kumbukumbu sahihi za matumizi ya mafuta," alisema.

# Wizara yaibua viwanja mbadala 3,992

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, ametaja hatua 10 zilizochukuliwa na wizara kutekeleza maagizo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ya kukabiliana na migogoro ya ardhi kwa Jiji la Dodoma ikiwamo tathmini ya awali kubaini madai ya viwanja mbadala 3,992.

Aidha, ameagiza watumishi 25 wa kujitolea waondolewe kwa kuzingatia maelekezo ya serikali.

Silaa aliwaambia waandishi wa habari jijini hapa jana kuwa Oktoba 3, mwaka huu Majaliwa alitoa maelekezo yaliyolenga kuboresha huduma za sekta ya ardhi Dodoma.

Alisema Jiji limebainisha viwanja 1,102 vilivyopo maeneo ya Nala Lugala (1,035) na Mkonze (97) kwa ajili ya fidia na baadhi ya wananchi wameanza kupewa.

"Halmashauri ya Jiji la Dodoma inaendelea na upimaji wa viwanja 5,000 katika eneo la Mahomanyika ambavyo vitatumika kufidia wananchi wenye madai, upimaji wa viwanja hivyo unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 31, mwaka huu," alisema.

Alisema Taasisi ya Kuzuia na Kuambana na Rushwa (TAKUKURU) inawachunguza watumishi tisa wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma waliosimamishwa kazi dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

"Wizara yangu itaendelea kuchukua hatua kwa watumishi wa sekta ya ardhi watakaokiuka maadili ya utendaji kazi," alisema.

Waziri huyo, alisema Wizara ya kushirikiana na Wizara ya Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imetoa maelekezo kadhaa ikiwamo kusitisha utaratibu wa upimaji shirikishi kwa jiji hilo na kuyasimamia mabaraza ya kata ili yawe na tija katika kushughulikia migogoro ya ardhi nchini.

Pia, alisema wizara inaendelea na uboreshaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kutunza Taarifa za Ardhi (ILMIS) ili kuboresha utoaji wa huduma, ikiwamo kurahisisha upatikanaji wa hatimiliki na utoaji huduma kwa wananchi kwa njia ya mtandao na yatakamilika mwishoni mwa mwaka huu.

"Wizara imeifanya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuwa Mkoa wa Ardhi kiutendaji ikiwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi atakayehudumia eneo hili na halmashauri zingine zitahudumiwa na kamishna msaidizi mwingine," alisema.

Kuhusu kliniki ya ardhi iliyofanyika hivi karibuni, Silaa, alisema imekuwa na matokeo chanya ambapo watu 3,056 walihudumiwa na hatimiliki 1,474 zilitolewa papo hapo.

"Maombi mapya 561 yalipokelewa, namba za malipo 1,674 zilitolewa na migogoro 774 ilishughulikiwa, kwa sasa wizara imeandaa utaratibu wa kutoa huduma kwa pamoja katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, utaratibu ambao utasimamiwa na wizara kwa kushirikiana na jiji kuanzia Oktoba 30, 2023," alisema.

Aliziagiza bodi zinazosimamia mipangomiji, upimaji ardhi na uthamini kuchukua hatua dhidi ya watalaamu na kampuni zilizokiuka maadili ya taaluma zao.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (kulia), akishirikiana na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), kuzindua mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji mapato na ufuatiliaji matumizi ya serikali ujulikanao GIMIS, uzinduzi huo ulifanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Wafanyabiashara wawapasha TRA kasumba ukusanyaji mapato

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JUMUIYA ya Wafanyabiashara Mkoa wa Singida wameitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupanua wigo wa kukusanya mapato na kuondokana na kasumba ya kurudi kwa wafanyabiashara wale wale kila mwaka kuwatoza kodi.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Florian Mallya, akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapa, alisema kumekuwa tatizo kwa TRA kuwatoza kodi wafanyabiashara wale wale kila mwaka huku wengine wenye sifa za kutakiwa kulipa wakiachwa.

"TRA ipanue wigo wa kukusanya kodi ili wasiwe wanatozwa wafanyabiashara wale wale na wigo ukipanuliwa hata kiwango cha mapato kitaongezeka na kama tatizo ni upungufu wa watumishi watumike viongozi wa vijiji na mitaa kuainisha wafanyabiashara wanaostahili kulipa kodi kwenye maeneo yao," alisema.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliwataka wafanyabiashara kuzingatia miongozo ya ulipaji kodi wanazostahili kulipa na utoaji wa stakabadhi za kieletroniki za EFD ili kukuza uchumi wa mtu mmoja na taifa.

Alisema Serikali imekuwa ikiboresha mazingira ya biashara kwa kuondoa tozo ambazo hazina tija ili kuongeza ukuaji wa biashara na uwekezaji hivyo wafanyabiashara waunge mkono jitihada za Serikali kwa kulipa kodi.

Serukamba, alisema Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa sekta za biashara na uwekezaji zinakua na kutoa mchango stahiki katika kukuza uchumi na pato la taifa kwa manufaa ya Watanzania.

Alisema ili kuhakikisha uboreshaji unakuwa na tija zaidi, Serikali imeanzisha idara ya uwekezaji, viwanda na biashara katika Sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kusimamia kwa karibu tasnia ya biashara nchini.

Alisema Mkoa wa Singida umebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi, hivyo sekta za umma na binafsi zinapaswa kufanya kazi pamoja ili kuwaletea wananchi maendeleo na kukuza uchumi.

"Ndoto yangu ni kuifanya Singida kuwa kitovu cha biashara na uwekezaji nchini na chombo muhimu kitakachonisaidia kutimiza ndoto hii ni Baraza la Biashara la Mkoa hivyo tuweke mpango mkakati wa kufanya kazi ndani ya miaka mitatu kwa kutangaza shughuli za biashara na uwekezaji," alisema.

Aliongeza kuwa dunia kwa sasa inakabiliwa na mabadiliko makubwa ya teknolojia ambayo yanasababisha kukua kwa haraka kwa uchumi, hivyo jitihada zinahitajika kujipanga kukabiliana nazo kwa kuimarisha mazingira wezeshi ya wafanyabiashara.

"Kasi hii ya ukuaji wa teknolojia imeendelea kuibua changamoto mbalimbali katika mazingira ya biashara ambazo zinahitaji utatuzi kwa njia ya majadiliano kuzipitia ufumbuzi zinazokabili ufanyaji wa biashara kwa kuzingatia miongozo iliyopo," alisema.





# DC ataja faida za upatikanaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakati

**Na Renatha Msungu,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila, amesema upatikanaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakati kutasaidia wakulima kujiinua kiuchumi pamoja na kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali wilayani hapa.

Aliyasema hayo wakati akitoa taarifa juu ya upatikanaji wa mbolea ya ruzuku wilayani Mbarali kwa wakulima wa mazao mbalimbali.

Alisema anaishukuru sana serikali kutokana na kuwapatia mbolea ya ruzuku wakazi wa eneo hilo, kwa sababu ni eneo linaongoza kwa matumizi sahihi ya mbolea ya ruzuku.

"Tunaishukuru sana serikali kutokana na kazi kubwa wanayofanya katika utoaji mbolea ya ruzuku hii itasaidia wakulima kuongeza uzalishaji," alisema Kanali Mwila.

Alisema hivi sasa wananchi wa wilaya hiyo wana uwelewa mkubwa katika matumizi sahihi ya mbolea pindi msimu wa kilimo unapowadia.

Akizungumza kwa niaba ya wanaushirika wa MAMCOS LTD, Ofisa Kilimo na Umwagiliaji wa Skimu ya Umwagiliaji ya Madibila, Hagai Kisunga, alisema mbolea ya ruzuku imeongeza tija kubwa sana kwa wakulima katika msimu uliopita wa kilimo.

Alisema kabla ya mtikisiko wa bei za mbolea wakulima katika skimu hiyo walikuwa wakivuna tani 7.5 hadi nane kwa hekta.

Alisema baada ya bei ya mbolea kupanda kwenye soko la dunia wakulima walishindwa kumudu bei ya mbolea na kutumia mifuko mitatu hadi minne badala ya mifuko ya mbolea nane hadi tisa ya kilo 50 kwa hekta moja na kusababisha kushuka kwa uzalishaji na tija.

Alifafanua kuwa baada ya serikali kuweka ruzuku ya mbolea msimu wa kilimo 2022/2023, wakulima walinunua mbolea na kuitumia kulingana na mahitaji ya zao, jambo lililochangia kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TFRA, Dk. Anthony Diallo, aliutaka uongozi wa chama hicho kuhakikisha wanachama wake wote wanajisajili katika daftari la wakulima na baadaye kwenye mfumo wa kidigitali wa mbolea ya ruzuku, ili waweze kunufaika na mpango huo wa mbolea za ruzuku unaotolewa na serikali.

**"Tunaishukuru sana serikali kutokana na kazi kubwa wanayofanya katika utoaji mbolea ya ruzuku hii itasaidia wakulima kuongeza uzalishaji," alisema Kanali Mwila.**

Mbali na hilo amewataka kuwahudumia wakulima wengine wasio wanachama ili kuisaidia serikali kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima wa pembezoni.

Mjumbe wa bodi, Patrick Mwalunenge, alisema kwa sasa chama chao kimejisajili ili kushiriki kwenye usambazaji wa mbolea za ruzuku na kueleza tayari wameshiriki mafunzo yaliyotolewa na TFRA.

Kutokana na hilo alisema msimu huu wakulima hawatapata shida ya upatikanaji wa mbolea ya ruzuku katika msimu ujao wa kilimo katika maeneo mbalimbali wilayani hapa.



Vijana wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya wakishirikiana kutengeneza baiskeli yenye mzigo wa ndizi baada ya kuharibika njiani jana, walipokuwa wanasafirisha ndizi hizo kutoka kwenye mashamba ya Kitengule. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Jeshi la Polisi latoa elimu ya kuzuia uhalifu kanisani, vyuoni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeanza mikakati ya kutoa elimu ya kukabiliana na matukio ya uhalifu kwenye taasisi za umma ikiwamo kanisani na kwenye taasisi za elimu ya juu, ili kupunguza kasi ya ongezeko la matukio hayo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alizindua rasmi utoaji wa elimu hiyo juzi ambapo alianzia katika Kanisa la Pentecostal Assemblies of God Mbeya Christian Centre.

Akiwa kwenye kanisa hilo, Kamanda Kuzaga alisema kukabiliana na uhalifu na wahalifu ni jukumu la kila Mtanzania na hivyo akawataka wananchi wote ndani ya mkoa huo kushiriki kwenye vita dhidi ya uhalifu.

Aliwataka waumini wa kanisa hilo kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu popote wanapobainika ili wadhibitiwe kabla hawajatekeleza uhalifu wao kwa maelezo kuwa uhalifu ukizidi kwenye jamii maendeleo yanakwama.

"Jukumu la kukabiliana na uhalifu ni letu sote, kwa hiyo nawaombeni wote tushirikiane kuwafichua wahalifu mahali popote watakapokuwa, ukiwaona toa taarifa ili sisi Jeshi la Polisi tutumie mbinu zetu kuwashughulikia," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema wataendelea kutoa elimu kwa makundi mengine ikiwamo kwenye misikiti, mikusanyiko mbalimbali ya wananchi pamoja na kwenye vituo vya mabasi ambako kunakuwa na watu wengi.

Alisema kwa sasa kuna polisi kata kwenye kata zote za Mkoa wa Mbeya ambao wanatakiwa kushirikiana na wananchi kukabiliana na uhalifu kwenye maeneo yao na hivyo akawataka wananchi kuwapa ushirikiano.

Askofu wa Kanisa la Pentecostal Assemblies of God Mbeya Christian Centre, Damianus Kongolo, alilishukuru Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya kwa jitihada zinazoendelea katika kutoa elimu mbalimbali kwa jamii.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa inayokabiliwa na matukio mengi ya uhalifu na hivyo jitihada za pamoja zinahitajika kukabiliana na uhalifu huo yakiwamo matukio ya mmomonyoko wa maadili kwa vijana.

# Wakulima Njombe wapewa elimu utambuzi mbolea feki

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA mkoani Njombe wamewekewa mkakati wa kuhakikisha wanapewa elimu ya kutambua mbolea feki, ili kukabiliana na hasara ambayo wamepata msimu wa kilimo uliopita.

Hatua hiyo ilielezwa na Meneja Masoko wa mbolea ya Itracom Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Amos Projest, wakati akizungumza na Nipashe katika maonesho ya nne ya viwanda vidogo vidogo kitaifa mkoani Njombe.

Alisema kuwa elimu itasaidia mbolea feki zisiingie kwenye mikono ya watu, pamoja na kutambua bidhaa feki ambazo zimeingizwa sokoni.

Alisema kwa mujibu wa TFRA Mkoa wa Njombe ni wa pili katika utumiaji wa mbolea.

Pia alitoa wito kwa wakulima kujitokeza kwa wingi kwenye maonesho hayo ili kupata elimu pamoja na wale ambao wamejisajiliwa katika mfumo wa ruzuku nao watahudumiwa.

"Na wale ambao hawajajisajili basi waende kwenye mamlaka ya serikali za mitaa kwa ajili ya kujisajili ili wapate kwa sababu msimu unakuja na wajiandae kwa ajili ya kupata mbolea bora lakini pia wajiandae kuzitumia kutokana na elimu watakayokuwa wamepata," alisema.

Wakizungumza na Nipashe, mmoja wa wakulima, Biana Mbawala mkazi wa Njombe, alisema msimu uliopita ulikuwa na maumivu kwa sababu walinunua mbolea feki na hivyo kuharibu mazao yao.

Alisema, "Umakini uongezwe kwa sababu msimu uliopita ulikuwa na maumivu, tulinunua mbolea lakini zilikuwa feki tulipata hasara na elimu tuliyopata hapa ni msaada mkubwa kwani sasa tutazitambua mbolea feki".



# Serikali yataja faida tatu za tamasha la vitabu

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohammed Mussa, amesema ujio wa tamasha la vitabu Zanzibar ni muhimu katika kuhamasisha wanafunzi kujenga utamaduni wa kusoma badala ya kupoteza muda mwingi kuangalia mitandao ya kijamii.

Aliyasema hayo wakati akifunga tamasha la kwanza la vitabu Zanzibar na kusema kuwa lazima kasi ya uandishi vitabu iende sambamba na hamu ya wananchi kuvinunua na kuvisoma.

Lela alisema Wizara imevutiwa na fikra ya kuanzishwa tamasha hilo ikiamini litaondoa uvivu kwa wanafunzi na watu wengine kuondokana na mitazamo hasi ya kwamba kusoma vitabu ni utamaduni wa wahenga ambao hauna nafasi katika kizazi cha sasa.

"Serikali itakuja na mbinu mbalimbali ili kufufua utamaduni wa kusoma vitabu kuanzia kwa wanafunzi ikiwemo kuingizwa kwenye mitaala ya elimu" alisema.

Alisema, huenda watoto wanapenda kusoma na ndiyo maana wanakesha katika mitandao kutafuta elimu mbalimbali, hivyo ni vyema jamii na wizara zibadili fikra zao kwa kuwafanya wasome vitabu kupitia teknolojia hiyo.

Aidha, alisema wizara itaangalia uwekezano wa kuingiza katika mitaala kuanzia kidato cha pili, sharti kwa wanafunzi kusoma idadi kadhaa ya vitabu na wanapomaliza kuwekwa katika rekodi ili iwe sehemu ya alama za ufaulu katika mitihani yao.


Waziri huyo aliwapongeza waandishi mahiri wa vitabu nchini akiwataja mshindi wa nishani ya tuzo ya Nobel, Profesa Abdulrazak Gurna, Ali Saleh, Adam Shafi, Mohammed Suleiman, Ali Rashid na wengine, kutokana na kazi zao kuitangaza Zanzibar, akiwataka wawashike mkono waandishi chipukizi.

Aliahidi kuwa wizara yake itaendelea kuliunga mkono tamasha hilo kuhakikisha linafanyika kila mwaka na kushirikisha waandishi kutoka nchi mbalimbali duniani.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Dk. Amina Ameir Issa, alisema tamasha hilo pia linaiongezea Zanzibar bidhaa zinazoweza kuuzika katika sekta ya utalii.

Aliwatia moyo waandishi wachanga wa vitabu ambao kazi zao zilioneshwa na kuuzwa katika tamasha hilo, sambamba na Umoja wa Washairi wa Pemba (UWAPE) na Chama cha Kuendeleza Washairi Zanzibar (CHAKUWAZA), kuendelea kukikuza Kiswahili kwa kutumia fani ya ushairi.

Washiriki wa hafla hiyo wakiwemo wanafunzi wa shule za sekondari, waliwataka wazazi na walezi katika familia wawe mfano kwa kusoma vitabu ili watoto nao wafuate nyayo zao.




Balozi Mdogo wa China, Zhang Zhisheng, akichagua kitabu katika maonyesho ya Tamasha la Vitabu mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Katibu CCM ataja faida uwekezaji Bandari ya Malindi

Na Mwandishi Wetu,
ZANZIBAR

KATIBU wa Idara ya Itikadi na Uenezi ya Kamati Maalum ya Chama Cha Mapinduzi Zanzibar, Mbeto Khamis Mbeto, amesema uwekezaji katika Bandari ya Malindi umelenga kuongeza ufanisi wa shughuli za upakuaji wa mizigo, kipato katika kipindi kifupi.

Mbeto alisema hayo katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa Magomeni Unguja akizungumza na wanachama wa CCM kuhusu umuhimu wa kuingia makubaliano na Kampuni ya AGL katika ukodishwaji wa Bandari ya Malindi Unguja.

Alisema serikali imechukua maamuzi hayo ambayo ni sahihi baada ya kuwepo kwa malalamiko ya muda mrefu ya kuzorota kwa shughuli za mizigo katika bandari hiyo.

Alisema wafanyabiashara walikuwa wakilalamika meli iliyobeba mizigo ikiwemo makontena kuchukuwa takribani siku 46 kabla ya kupata nafasi ya kufunga gati na kuanza kushusha mizigo.

"Hizo ndiyo sababu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuingia ubia na Kampuni ya AGL kutoka Ufaransa kwa ajili ya kuleta ufanisi wa kazi na kupunguza malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara" alisema.

Mwakilishi wa Magomeni ambae pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Jamal Kassim Ali alisema maslahi yote yamezingatia katika uwekezaji wa Bandari ya Malindi ambapo serikali itapata mgawanyo wa mapato kwa asilimia 30.

Aidha, alisema uwekezaji wa Bandari umefanywa kwa Bandari ya Malindi pekee, huku serikali ikiendelea na kazi ya ujenzi wa bandari nyingine ziliopo mkoani Pemba na kuwa lango kuu la kiuchumi katika Afrika ya Mashariki.

# TAMWA yataka mkakati wa kuwanusuru vijana kimaadili

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, (TAMWA Zanzibar) kimesema kuna haja ya kuandaliwa kwa mkakati wa kitaifa wa kubadilisha tabia za vijana, ili kuwaokoa katika dimbwi la vitendo viovu ikiwemo vya udhalilishaji.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa aliyasema hayo visiwani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari na kusema vijana wengi wanajihusisha na masuala ya udhalilishaji na hivyo jitihada za makusudi zinahitajika ili kuwabadilisha kimawazo.

Alisema kwa mujibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kuanzia Julai hadi Septemba, mwaka huu watu 24 wamekutwa na hatia mahakamani kwa kufanya makosa ya udhalilishaji na kupewa adhabu za vifungo, kwamba asilimia 58.3 ni vijana wa umri wa miaka 18 hadi 29.

"Takwimu hizo pia zinaonesha watu ambao bado wapo mahabusu kesi zao zinaendelea ni 48 ambapo kundi hilo la miaka 18 hadi 29 pia linaongoza ambalo linafanya asilimia 54" alisema.

Aidha, aliitaka serikali kuandaa mkakati wa kuelimisha vijana kupitia maeneo mbalimbali ikiwemo viwanja vya michezo, shule lakini pia kutoa taaluma kwa wazazi na walezi jinsi ya kuwafahamisha watoto wa kiume namna ya kuheshimu watoto wa kike na wanawake.

Alisema, pia takwimu zinaonesha kuwa masuala hayo ya udhalilishaji yanawaathiri watoto zaidi ambapo katika matukio 157 kwa Julai hadi Septemba yaliyoripotiwa, watoto ni 122 sawa na asilimia 77 katika maeneo kadhaa hasa kubakwa, kukashifiwa na kulawitiwa.

"TAMWA pia inawashauri sana vijana kushtushwa na taarifa hizi na hivyo kujipangia mipango madhubuti ya kutokuingia katika vitendo hivi ikiwemo kuacha kufuata vishawishi, kutokuendekeza mihemuko na pia kujidhibiti dhidi ya matumizi mabaya ya mitandao" alisema.

Hata hivyo, alisema ni vyema vijana wakaelewa kuwa katika vijana waliotiwa hatiani kwa makosa ya udhalilishaji wengi wao wamehukumiwa kutumikia adhabu ya zaidi ya kifungo miaka 11 jela, hivyo kupoteza kipindi kirefu cha nguvu zao katika magereza badala ya kutumia kujipanga na maisha yao.

Alisema: "Tunaipongeza Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kwa kutoa takwimu za matukio ya udhalilishaji kila mwezi ambapo utoaji huu wa takwimu utasaidia kujua umri wa wanaofanya makosa mbalimbali na hivyo kuona jinsi gani nchi inaweza kujipanga katika kubadilisha tabia za makundi yaliyo hatarishi zaidi".

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP




**VIVIAN HENRY MAPUNDA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.2325/0648** iliyotolewa na CANOSA SEKONDARI mwaka 2023. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/ILA/28499/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAID HAMISI SALUMU** anatangaza kupotea kwa cheti cha TECHNICIAN CERTIFICATE IN CLINICAL MEDICINE chenye namba ya usajili **NS1077/0076/2014** kilichotolewa na CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI ELIJERRY mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **TAN/MUH/RB/204278/2023**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**GIDEON PHAUSTINE MWANISAWA** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 430986** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 18/10/2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/6036/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JANETH THOMAS MWABWINA**, anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Sita Chenye Index Namba **S.0681/0628** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari Ivumwe Mwaka 2022. Yeyote atakayekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **PHQ/IRI/IRI/2403/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEOFREY PAUL NICODEMUS** anatangaza kupotea kwa cheti cha **TECHNICIAN CERTIFICATE IN CLINICAL MEDICINE** chenye namba ya usajili **NS2143/0055/2014** kilichotolewa na CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI ELIJERRY mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **TAN/MUH/RB/204278087/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ROSEMIRIAM NYABUREGESI NGARA** anatangaza kupotea kwa cheti cha TECHNICIAN CERTIFICATE IN CLINICAL MEDICINE chenye namba ya usajili **NS0630/0042/2015** kilichotolewa na CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI ELIJERRY mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **TAN/MUH/RB/204278083/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(MCA)**

**Mahakama ya mwanzo Arusha Mjini**
**Wilaya ya Arusha**

**MADAI NAMBARI 138 YA 2023**

**Mdai: Francis Christopher Yalomba**

**Amdai**

**Mdaiwa: Mwanakombo Mbaruku Ally**

**Kwa Mwanakombo Mbaruku Ally wa Dar- Es- Salaam kwa kuwa mdai wadai ameleta /wameleta madai yoke /yao kwamba ( Eleza hapa habari za madai).**
**Fika mahakamani bila kukosa kujibu madai ya Talaka, mgawanyo wa mali na matunzo ya watoto.**

Kwa hiyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria mahakama hii siku ya Alhamis tarehe 19/10/2023 saa 2:30amasubuhi/ alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/ wenu na hati zote zinazohusu shauri hili kwa jaili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria /hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hili itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii ya tolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 2/10/2023.

2/10/2023

**Hakimu /Hakimu mahakama ya Mwanzo .**

Hakimu / Hakimu Mahakama ya Mwanzo

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 74/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU OMARY SALUM MALEDA wa NKUHUNGU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**
**MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA SALUM OMARY SALUM**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 17 Mwezi 10 Mwaka 2023.

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 461 LA 2023**

**JUDITH CHARLES CHOWAJI NA WENZAKE 2**
**.............MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**(1) ASSELA MARCELLUS LUENA**
**(2) KABANGO GENERAL BUSINESS....MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**(1) ASSELA MARCELLUS LUENA**
**(2) KABANGO GENERAL BUSINESS**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**JUDITH CHARLES CHOWAJI NA WENZAKE 2** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 31/10/2023 saa 3:00 asubuhi mbele ya **Mh. J.W. SILLAS.** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 9 Mwezi 10, 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 17/2023**

**(Asili ya shauri namba 94/2019 kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba wilaya ya Songea)**

**MALISELA DESDERIUS SANGA...MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ZOOH MOHAMED KISALELE....MJIBU MAOMBI**

**COSMA IVO KISALELE.............MJIBU MAOMBI**

**OTHMAN MAJIMOTO............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Zooh Mohamed Kisalele unataarifiwa kuwa mleta maombi amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako.Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 09/11/2023 saa 2:00 asubuhi.Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ONE ACRE TANZANIA LIMITED**
WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HILUX D/CABIN RANGI NYEUPE YENYE USAJILI **T195DFH,** ENGINE **NO:2KDA786778**
YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE
POLISI TAARIFA
**PHQ/IRI/IRI/1980/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMANUEL JOHN MUTABOYERWA**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALPHARD** yenye usajili namba **T 666 CAR.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DR/KIN/25538/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YUSUPH HAMIDU MOHAMED**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **COROLLA AXIO-TOYOTA** yenye usajili namba **T 912 DJE,** CHASSIS NAMBA: **NZE14160554994** na ENGINE NAMBA: **1N2C782155.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/29110/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 1554/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU MEGHA KANAIVAL SHUMLABHAI WA ILALA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA**
**NA CHETAN VINOD BHATT**

**TANGAZO**
**( kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 16 Mwezi 10 Mwaka 2023

HAKIMU

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DISMAS ARNOLD MARIKI**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 239 AXK - TOYOTA STATION** WAGON yenye Chassis No. **AE1150007823.** Engine No. **7AAG049682.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/ARU/ARU/5121/2023.**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0745 700 710.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Misaada yaanza kumiminika Gaza

**TEL AVIV,** Israel

MSAFARA wa tatu wa malori yaliyobeba msaada umeingia Ukanda wa Gaza kutoka Misri kupitia kivuko cha Rafah, baada ya mengine 20 yaliyoingia Jumamosi na Jumapili.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Msalaba Mwekundu, msaada huo wa tatu uliingia Gaza jana, huku ikieleza kuwa uhitaji wa msaada wa kibinadamu ni kama janga katika ukanda huo.

**Siyo kutia chumvi kusema ni janga huko Gaza.**

Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu ilikaribisha kuwasilishwa kwa misafara miwili ya kwanza ya misaada huko Gaza, licha ya kusema kwamba kiasi kilichoingia mpaka sasa katika ukanda huo ni kama tone tu kutokana na idadi iliyopo ya watu wenye uhitaji.

Akizungumza na BBC, msemaji wa shirika la kutoa misaada Imene Trabelsi, alisema kuna haja ya kuwa na mpango endelevu wa kuwasilisha vifaa, akidokeza kwamba idadi kubwa ya watu wa Gaza walikuwa wakitegemea misaada kabla ya mzozo wa hivi karibuni kuzuka.

Trabelsi alieleza kuwa familia zilizolazimishwa kutoka katika nyumba zao zinalala mitaani bila vitu muhimu kama vile blanketi kwasababu makazi tayari yamejaa.

Alisema "Siyo kutia chumvi kusema ni janga huko Gaza." Licha ya msemaji wa IDF wiki iliyopita kupendekeza kuwa hakuna mgogoro wa kibinadamu huko Gaza.

Aidha, Jeshi la Ulinzi la Israeli (IDF) lilisema katika saa 24 zilizopita, lilipiga shabaha zaidi ya 320 katika ukanda wa Gaza. Na kwamba kulishuhudiwa picha za uharibifu huko kusini mwa ukanda huo.

Msemaji wa Jeshi la Israel, Daniel Hagari, alisema kuwa IDF ilishambulia vikundi vinane vya magaidi nchini Lebanon katika muda wa saa 24 zilizopita.

Pia alisema vikundi saba kati ya hivyo vilipigwa kabla ya kufanikiwa kurusha makombora ya vifaru, kwamba seli 20 za Hezbollah zilishambuliwa tangu mapigano yalipozuka kwenye mpaka mapema mwezi huu. **BBC**



Sehemu ya misaada ya kibinadamu iliyoingizwa ukanda wa Gaza hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

## Macron kuzuru Israel leo

**PARIS,** Ufaransa

IKULU ya Élysée imebainisha kuwa Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron anatarajiwa kufanya ziara Mjini Tel Aviv leo ili kukutana na Waziri Mkuu wa Israeli Benjamin Netanyahu.

Ziara ya mkuu wa nchi ya Ufaransa imekuja baada ya mashambulizi ya Hamas katika ardhi ya Israel, ambayo yalisababisha vifo vya zaidi ya watu 1,400 wakiwemo raia 30 wa Ufaransa. Ikielezwa kua watu saba wa Ufaransa bado hawajapatikana.

Kiongozi wa serikali ya Israel alitangaza jana, kuhusu ujio wa ugeni huo, kupitia mtandao wa X (zamani Twitter) na kwamba ziara hiyo ya Rais wa Ufaransa itahusisha pia na ya waziri mkuu wa Uholanzi Mark Rutte.

Aidha, viongozi wengine wakuu waliotembelea taifa hilo tangu kuzuka kwa machafuko ni Rais wa Marekani Joe Biden, Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, Waziri Mkuu wa Uingereza Rishi Sunak, na mkuu wa serikali ya Italia Giorgia Meloni.



Hata hivyo, Rais Macron kwa upande wake alisema akirejelea kauli yake siku ya Ijumaa kwamba atazuru Mashariki ya Kati ikiwa ataweza kupata mambo muhimu kwa ajili ya kanda hiyo kutokana na ziara hiyo.

Vile vile, alitaja miongoni mwa mambo hayo ikiwemo usalama wa Israel, mapambano dhidi ya makundi ya kigaidi, kusitishwa kwa mgogoro na kuanza tena mchakato wa kisiasa kuelekea suluhisho la serikali mbili, Israeli na Palestina.

Pia kiongozi huyo alionyesha kuunga mkono bila kushindwa kwa Waisraeli, juu ya haki yao ya kujilinda, akitoa wito wa kusitisha mashambulizi ya Israeli dhidi ya Hamas huko Gaza.

Ilibainishwa kuwa Rais Biden alijadili vita kati ya Hamas na Israel kwa njia ya simu juzi na Rais Macron, Justin Trudeau wa Canada, Olaf Scholz, Giorgia Meloni na Rishi Sunak. **RFI**

## Machafuko mapya yashuhudiwa DRC

**MASISI,** DRC



MACHAFUKO mapya yameibuka mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) yakihusisha waasi wa M23 dhidi ya waasi wanaounga mkono serikali, jambo linalotajwa kuchochea wasiwasi katika mji wa kimkakati wa Masisi.

Kwa mujibu wa mamlaka ya Mji wa Masisi, mapigano hayo yalishuhudiwa juzi, na kukiuka mkataba wa usitishaji mapigano uliodumu kwa miezi kadhaa.

Mmoja wa wakazi wa eneo husika, alisema kuwa wamejificha kanisani kutokana na kwamba waasi wa M23 wako katika eneo la Kitshanga tangu juzi.

Kwa mujibu wa mfanyakazi wa afya ambaye hakutaka jina lake litajwe, katika mapigano hayo watu kadhaa walijeruhiwa na kupelekwa hospitali, huku akieleza kuwa "Asubuhi hii, hakukuwa na wapiganaji wowote, lakini bado tunaogopa kutoka nje".

"Waasi wako Kitshanga na tunajaribu kutafuta njia ya kuukomboa mji huo," duru ya usalama iliiambia shirika la habari la Ufaransa, AFP, pia kwa sharti ya kutotajwa majina.

Msemaji wa kundi moja la waasi wanaojiita wazalendo wanaopambana na waasi, alisema vita hivyo havitakoma na vitaendelea

Kwa mujibu wa duru ya usalama, mapigano yalikuwa yakiendelea Jumapili katika eneo jirani la Rutshuru, Kitshanga mji unaopatikana eneo la Masisi, kilometa 80 kaskazini magharibi ya Goma, mji mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini.

Ilielezwa kuwa mara kadhaa mji wa Kitshanga umedhibitiwa na mamlaka tofauti tangu mwanzo wa mwaka huu, huku mapigano yakizuka tena wiki tatu zilizopita kutokana na mkataba dhaifu wa miezi sita wa kusitisha mapigano.

Kundi la waasi la M23 linaloongozwa na Watutsi na linaloungwa mkono na Rwanda liliudhibiti mji huo mwezi Januari, likiendeleza harakati zake za kuyateka maeneo makubwa ya ardhi.

Mwanzoni mwa Oktoba, mji wa Kitshanga ulitoka mikononi mwa kikosi cha kimataifa kilichotumwa na Jumuiya ya Afrika Masahriki, ambacho kiliweka eneo ambalo halikuruhusiwa shughuli za kijeshi kati ya makundi ya waasi, na kuingia mikononi mwa waasi wa eneo hilo na kwa saa 24 ukadhibitiwa na kundi la M23, kabla ya waasi hao kuondoka mjini humo.

Pia mwezi Oktoba, jeshi ambalo linadai kusimamia usitishaji mapigano kutokana na amri ya mpatanishi wa kikanda, lilikuwa limeandaa safari na vyombo vya habari kwenda mjini Kitshanga wiki moja kabla ya mji huo kuanguka tena mikononi mwa waasi. **DW**

# KITAMBI ATWISHWA ZIGO ZITO LILILOMSHINDA KAZE NAMUNGO

**Na Saada Akida**

BAADA ya Kocha Cedric Kaze kujiuzulu kukinoa kikosi cha Namungo FC, uongozi wa klabu hiyo umesema timu itakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Denis Kitambi, ambaye atasimamia mechi ijayo ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC wakati ukisaka kocha mwingine.

**Awali, Kitambi alikuwapo kwenye benchi hilo kama kocha msaidizi akisaidiana na Kaze kabla ya kujiuzulu kwa sababu ya mwenendo mbaya katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Namungo FC, Namlia Kindamba, alisema baada ya kuona taarifa za kujiuzulu kwa Kaze uongozi umeamua timu kuendelea kubaki chini ya Kitambi akishirikiana na Kocha wa viungo, Shadrack Nsajigwa, hadi hapo watakapofanya maamuzi mengine

Alisema kutokana na kujiuzulu kwa Kaze, hawatapata athari yoyote ya maandalizi ya mchezo wao ujao dhidi ya Azam FC, na wanaima kubwa ya kufanya vizuri wakiwa na Kitambi

"Tunaheshimu maamuzi ya Kaze kujiuzulu, maisha mengine yanaendelea na kikosi kitaondoka kesho (leo), kuelekea Dar es Salaam kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Azam FC.

"Kocha Kitambi na Nsajigwa wataendelea na majukumu yao, ninaimani watafanya vizuri kwenye mechi yetu dhidi ya Azam FC kama ilivyo kwa msimu uliopita kuchukua alama tatu kwenye dimba la Azam," alisema Kindamba.



Aliongeza kuwa wanaingia Dar es Salaam mapema kwa lengo la kupata siku mbili za kufanya mazoezi kabla ya kukutana na Azam FC.

Alisema wanatambua haitakuwa mechi rahisi kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao hao na ugumu wa ligi kwa msimu huu, lakini wamejipanga kupambana kutafuta pointi katika kila mchezo ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye msimamo wa Ligi hiyo.

Namungo FC inashika nafasi ya 14 kutoka chini ikicheza michezo sita ikipoteza mitatu na sare tatu hajashida mechi hata moja.

## SITOWAANGUSHA...



Bondia wa Ngumi za Kulipwa nchini, Abdallah Pazi maarufu Dullah Mbabe (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuelekea pambano lake na Bondia Erick Katompa kutoka DR Congo linalotarajiwa kufanyika kesho, Jumatano jijini Arusha, lengo likiwa ni kutangaza utalii. Katikati ni Mkurugenzi wa Kampuni ya kuandaa mapambano ya ngumi nchini, Sophia Mwakagenda na mshauri wa masuala ya ngumi, Mhandisi John Chaggu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Ngome FC yatoa sababu kuinyoa KVZ

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kuonja ushindi kwa mara ya kwanza tangu Ligi Kuu Zanzibar ianze msimu huu, Kocha Msaidizi wa Ngome FC, Abdilah Juma, ametoa sababu zilizochangia kuvuna alama zote tatu juzi dhidi ya vinara wa ligi hiyo, KVZ SC.

Katika mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Mau A, Ngome FC iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 huku hicho pia kikiwa kipigo cha kwanza kwa KVZ tangu kuanza kwa msimu huu.

Magoli ya Ngome FC yalipachikwa nyavuni na Omar Thani dakika ya 60 na 90, wakati bao la kufutia machozi kwa KVZ SC lilifungwa na Suleiman Mwalim dakika ya 26.

Kabla ya ushindi huo Ngome FC ilikuwa ikiburuza mkiani kwenye msimamo, lakini sasa imepanda kwa nafasi mbili kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 baada ya kufikisha alama tano.

Akizungumza na Nipashe Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Juma alisema kwa mara ya kwanza wamepata ushindi kwa timu ambayo haijawahi kufungwa tangu ligi hiyo ianze msimu huu.

Alisema kupata ushindi huo kutoka kwa vinara wa Ligi Kuu Zanzibar, ni juhudi zilizofanywa na wachezaji wa timu hiyo kutokana na kuendelea kufanyia kazi mapungufu yote wanayoyaona kwa kila mchezo.

Alisema hawezi kusema kuwa timu yao imeimarika kwa asilimia 100, bali imepiga hatua ya kiuchezaji ikilinganishwa na michezo iliyokuwa mbele yao.

Alisema kupitia mchezo huo, aliona kwa kiasi kikubwa timu yake itafanya vizuri hata michezo iliyokuwa mbele yao.

"Tulijitahidi kuingia kwa kupambana ili kuhakikisha tunapata alama tatu muhimu, na tulijua tunaenda kukutana na timu ngumu ambayo ni vinara wa Ligi Kuu na tulicheza kwa tahadhari sana," alisema.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa KVZ SC, Ali Mohmed, alisema timu yake ilicheza vizuri, lakini bahati haikuwa upande wao.

Alisema magoli yote mawili waliyofungwa ni makosa madogo sana yaliyofanywa na safu ya ulinzi ya timu yao katika harakati za kuokoa.

Hata hivyo, alisema wanajipanga katika mchezo wao wa nane dhidi ya KMKM utakaochezwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Mau A.

# Wasanii Afrika Mashariki wakutana Tamasha la Utamaduni

**Na Frank Monyo**

WASANII wa muziki wa Bongo Fleva kutoka Tanzania, Kenya na Uganda, wamekutana kwenye jukwaa moja na kushusha burudani katika Tamasha la Muziki na Utamaduni wa Kiafrika la Serengeti Lite Oktobafest.

Tamasha hilo lilifanyika mwishoni mwa wiki katika fukwe za Coco na kuudhuriwa na wapenda burudani kutoka Afrika Mashariki.

Wasanii waliotoa burudani hiyo ni Nyamari Ongegu maarufu Nyanshiski kutoka Kenya, Jose Chameleon kutoka Uganda, Ali Kiba, Bill Nas, Chino, G Nako, kutoka Tanzania pamoja na wabunifu wa mavazi kama vile Makeke International kutoka Tanzania.

Meneja wa Chapa ya Serengeti Lite na Serengeti Premium Lager, Esther Raphael, alisema maadhimisho ya tamasha hilo la muziki na utamaduni ni jukwaa lililowezesha vijana wa Afrika Mashariki kupata fursa za biashara kupitia burudani na ubunifu mbalimbali.

"Zaidi ya hayo, tamasha hili linaonesha jinsi bia inaweza kutumika kama daraja, kuunganisha tamaduni na watu mbalimbali wa Afrika Mashariki kwa lugha ya muziki," alisema.

Meneja Mawasiliano na Uendelevu Serengeti Breweries Limited (SBL), Rispa Hatibu (pichani), alisema fahari ya tamasha hilo pia ni kuzingatia utunzaji wa mazingira.

"Serengeti Lite Oktobafest lilikuwa tamasha lenye kutunza mazingira bila taka zozote, ambapo mazingira yalipewa kipaumbele. Timu yetu ya waokota taka ilifanya kazi kwa bidii kuhakikisha mazingira safi ni kila wakati wakati wa tamasha katika fukwe za coco," alisema.



ZISIKUPITE

## DE BRUYNE KUTOONGEZEWA

KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne, 31, huenda asipewe ofa ya kuongezewa mkataba katika Klabu ya Manchester City iwapo rekodi yake ya majeruhi itazidi kuwa mbaya. ***(Football Insider)***

## ANDRE AWINDWA ARSENAL

ARSENAL inataka kumnunua kiungo wa kati wa Fluminense, Mbrazil Andre, 22, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Fichajes)***

## MUSIALA AWINDWA CITY

KLABU ya Manchester City inachunguza uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Jamal Musiala, 20, huku Liverpool pia wakimtaka mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

## MESSI HAFIKIRII MKOPO

MSHAMBULIAJI wa Inter Miami, Lionel Messi, 36, hafikirii mkataba wowote wa mkopo kuanzia sasa hadi msimu mpya wa Ligi Kuu ya Marekani utakapoanza Februari licha ya kuhusishwa na Barcelona. ***(Fabrizio Romano)***

## CHELSEA NA OSIMHEN

CHELSEA inaendelea kufuatilia hali ya fowadi wa Nigeria, Victor Osimhen, 24, pale Napoli licha ya tetesi kumhusisha na Liverpool. ***(TeamTalk)***

## SILVA KUTUA FLUMINENSE

KLABU ya Fluminense ya Brazil inajiandaa kumnunua mlinzi wa Chelsea, Thiago Silva, 39, huku kukiwa na uvumi kwamba Mbrazil huyo atakondoka Stamford Bridge mwishoni mwa msimu huu. ***(Fichajes)***

## DAVIES GHARAMA KUBWA

MLINZI wa kushoto wa Bayern Munich na Canada, Alphonso Davies, ataigharimu Real Madrid angalau pauni milioni 40 ikiwa klabu hiyo ya LaLiga inataka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Bild)***

## AWANIWA LUTON

KLABU ya Luton italazimika kulipa angalau pauni milioni 5.5 kwa kiungo wa Ecuador, Oscar Zambrano, 19, huku klabu yake ya LDU Quito ikishikilia ofa bora zaidi. ***(Sun)***

## BUTLAND ATAJWA RANGERS

KLABU ya Rangers inataka ofa ya angalau pauni milioni tano ili kumuuza kipa wao, Jack Butland, 30. ***(TeamTalk)***

## VIKCERS HANA HARAKA

MLINZI wa zamani wa Tottenham Hotspur, Cameron Carter-Vickers, 25, hana haraka ya kurejea Ligi Kuu England, huku Mmarekani huyo, ambaye kwa sasa yuko Celtic kwa mkopo, akiendelea kuzua gumzo la uhamisho. ***(Goal)***

## KONE MWAKA MMOJA

BORUSSIA Monchengladbach itaanzisha kipengele cha kuongeza mkataba na kiungo Mfaransa, Manu Kone, 21, kwa mwaka mmoja ili uendelee hadi 2026. ***(Rheinische Post, via Get German Football News)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA SASA YAANDAA MECHI KUMUAGA MESSI

**BARCELONA,** Hispania

MKURUGENZI wa michezo wa Barcelona, Deco amefichua kuwa klabu hiyo inakusudia kuandaa "mchezo wa kumuaga" Lionel Messi.

**Messi ndiye mwanasoka bora zaidi kuwahi kuichezea Barcelona, na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo - akiwa na mabao 672 katika mashindano yote na mfungaji bora wa muda wote – akicheza mechi 778 katika mashindano yote katika miaka yake 17 ndani ya kikosi cha kwanza.**

Klabu hiyo ililazimika kumruhusu mchezaji huyo kuondoka mwaka 2021 kutokana na matatizo ya kifedha, huku Messi akitumia misimu miwili katika Klabu ya Paris Saint-Germain.

**Hakika atacheza mechi ya kuaga Barcelona, lakini itakuwa lini...**

Baada ya kumalizika kwa mkataba wake wa miaka miwili katika klabu hiyo ya Ligue 1, Barca walijaribu kumsajili tena Messi, lakini hawakuweza kutokana na matatizo ya kifedha.

Kwa hiyo, Messi alihamia Inter Miami ya Ligi Kuu ya soka Marekani (MLS), ambapo amemaliza kampeni yake ya kwanza akifunga mabao 11 katika mashindano yote.

Bila kufuzu kwa hatua ya mtoano, uvumi umeenea kuhusu uwezekano wa kurejea Ulaya kwa mkopo wakati wa msimu wa baridi.

Mshambuliaji huyo maarufu tangu wakati huo amefutilia mbali uvumi huo, hata hivyo akizungumza na Lance, Mkurugenzi wa Michezo wa Barcelona, Deco amefichua kwamba mashabiki wanaweza kutarajia kuona Messi akirejea katika rangi ya klabu hivi karibuni.

"Nadhani kutakuwa na mchezo wa kumuaga, lakini labda katika uwanja mpya ukiwa tayari. Daima atakuwa sanamu mkubwa katika historia ya klabu. Klabu ilikuwa na sanamu kubwa, kama Cruyff, lakini labda ndiye mkuu kuliko wote.

"Hakika atacheza mechi ya kuaga Barcelona, lakini itakuwa lini, hatujui. Atacheza, na tunatumaini atacheza kwa miaka zaidi, kwa sababu watu wanaopenda soka, wale wanaopenda, watafurahi kumuona akiwa na furaha."

Barcelona wanatarajia kurudi kwenye uwanja wao wa Camp Nou Novemba 2024 baada ya kukamilika kwa ukarabati wake.

# NAVILLE: PRESHA NI KUBWA KWA RAYA



**LONDON,** England

GARY Neville anaamini presha inaanza kumpata golikipa namba moja wa Arsenal, David Raya na anazidi kufanya 'makosa'.

Raya alikuwa na wakati mgumu katika mechi ya Arsenal kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lens na kujiamini kwake kulipata pigo jingine alipofungwa na Mykhailo Mudryk katika sare ya mabao 2-2 ya Arsenal dhidi ya Chelsea kwenye Ligi Kuu England, Jumamosi.

Neville, ambaye alikuwa mchambuzi katika mechi hiyo ya dabi ya London, anahisi kwamba kiwango cha Raya tangu kumpokonya namba moja Aaron Ramsdale kinaanza kumpa presha raia huyo wa Hispania.

"David Raya alianza soka lake pale Arsenal vema, lakini baadaye akawa na mchezo mbaya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya (dhidi ya Lens) ikifuatiwa na kipindi cha kwanza dhidi ya Manchester City," alisema Neville wakati akizungumza na Sky Sports.

"Sasa presha inazidi kuwa kubwa kwake," alisema.

"Ni nafasi ngumu zaidi kucheza na hakika unapokuwa katika moja ya klabu kubwa kwenye ligi, unaangaliwa zaidi - hasa kama wewe ni golikipa.

"Mikel Arteta ameunda hilo, tuwe wazi na hali ya Ramsdale na Raya. Si kawaida, lakini inaweza kufanya kazi.

"Sijawahi kuamini inaweza, na ninaamini tunaona mbele ya macho yetu changamoto zilizopo kwa sababu sasa, kutakuwa na shinikizo.

"Aaron Ramsdale hakuwa amefanya makosa mengi mwanzoni mwa msimu. Raya sasa ameanza kufanya makosa."

Ramsdale hajaficha kufadhahika kwake kwa kushindwa kuichezea Arsenal, si haba kwa sababu anahofia nafasi yake katika kikosi cha England kwa ajili ya michuano ya Ulaya msimu ujao.

# Mourinho aishangaa kadi yake nyekundu

**ROME,** Italia

JOSE Mourinho amesema haelewi ni kwa nini alioneshwa kadi nyekundu kwa kutoa ishara ya kulia kuelekea mwisho wa ushindi wa Roma wa bao 1-0 dhidi ya Monza Jumapili.

Bao la dakika ya 90 kutoka kwa Stephan El Shaarawy liliwahakikishia Roma ushindi dhidi ya Monza, ambao walikuwa na wachezaji 10 baada ya Danilo D'Ambrosio kutolewa kipindi cha kwanza.

Mourinho alioneshwa kadi nyekundu dakika za lala salama baada ya kuonekana akionesha ishara ya kulia kuelekea makocha wa Monza.

"Sijui kwa nini nilipata kadi nyekundu, nilionesha ishara tu kwa benchi, hakuna hata neno moja," alisema Mourinho.

"Benchi la Monza liliweka shinikizo kubwa kwa mwamuzi; hawakupaswa kuwa na tabia kama hiyo."

Akiwa na kadi nyekundu, Mourinho hatakuwa kwenye benchi katika mechi inayofuata ya ligi ya Roma ugenini dhidi ya klabu yake ya zamani Inter Milan.

Licha ya kuonekana kuwakejeli wakufunzi wa Monza, Mourinho alitoa sifa tele kwa timu ngeni.

"Hawakustahili kupoteza mchezo," alisema Mourinho.

"Timu yangu ilikuwa kwenye matatizo kila mara, tulifanya makosa mengi na tuliteseka. Ulikuwa ni mchezo wenye kiwango cha chini cha kiufundi lakini chenye hisia za juu."





# *Hernandez akunwa na kinda Marc Guiu*

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, alimsifu Marc Guiu asiye na woga baada ya kijana huyo mwenye umri wa miaka 17, kuingia akitokea benchi na kufunga bao pekee katika mchezo wake wa kwanza dhidi ya Athletic Bilbao Jumapili.

Guiu alitambulishwa zikiwa zimesalia zaidi ya dakika 10 kwenye Uwanja wa Olympic akitelezesha ushindi baada ya sekunde 33 kwa kulishwa na Joao Felix na kuipa Barca ushindi wa bao 1-0 kwenye Ligi Kuu Hispania.

"Marc ni mtoto kutoka akademia na alifanya mabadiliko," alisema Xavi katika mkutano na waandishi wa habari.

"Nina furaha kwake na kwa pointi tatu, ambazo ni muhimu sana.

"Nilimfikiria wakati huo kwa sababu ni mfungaji wa mabao, ana cheche na mimi binafsi nampenda, sina tatizo kuangalia tuna nini ndani, kinyume kabisa nataka kuwapa imani ambayo nilipewa nikiwa na umri wa miaka 17 na 18."

Guiu ndiye chipukizi wa hivi karibuni zaidi kutokea katika akademi ya Barcelona na kuleta matokeo kwenye kikosi cha kwanza.

Lamine Yamal (16) na Fermin Lopez (20), pia wamefuzu msimu huu, na kufunga mabao muhimu kwenye mechi walizocheza dhidi ya Mallorca na Granada msimu huu. Gavi (19) na Alejandro Balde (20), wote wamejiimarisha kama wachezaji wa kikosi cha kwanza kwa Barca.

"Kitu ambacho kinanishangaza na kizazi hiki ni kwamba hawana hofu," aliongeza Xavi kuhusu vijana hao wa Barca.

"Labda ilikuwa tofauti katika siku yangu. Wana cheche hiyo. Wananitazama kwa uso unaosema: 'Niweke, nitakuonesha kwamba itaenda vizuri.' Tunapowaweka, wapo tayari, wanaonesha tabia na ushujaa.

"Niliiona kwa Gavi, Balde, Lamine, Fermin... na niliiona kwa Marc. Hakukuwa na hofu usoni mwake. "Nilimwambia atapata nafasi moja, akapata nafasi moja na akaichukua, nilihisi yuko tayari, nina furaha sana kwa Marc, ni mtoto mzuri anayefanya kazi kwa bidii.

Guiu, ambaye alijiunga na akademi ya klabu hiyo mwaka wa 2013 na ni mchezaji wa kimataifa wa Hispania chini ya umri wa miaka 17.

HABARI MICHEZO

# Yanga, Aziz Ki wakaa kileleni

INATOKA UKURASA 24

mabeki wawili wa Azam FC na kipa Iddrisu baada ya kuona hivyo alijaribu kutoka langoni kumkabili, lakini mfungaji aliupiga mpira kwa mguu wa kushoto kwa ufundi kama anapiga krosi, mpira ukajaa wavuni kwenye 'engo' ya pili.

Azam FC ilisawazisha bao dakika 10 baadaye kupitia kwa kiungo mshambuliaji raia wa Gambia, Jibril Sillah.

Aliupata mpira akiwa wingi ya kulia na kukimbia nao, akawapasia wenzake ambao walimrejeshea akiwa ameingia ndani kidogo ya eneo la hatari, kabla ya kuwahadaa mabeki wa Yanga na kuachia shuti la mguu wa kushoto na kutinga kushoto kwa kipa Djigui Diarra, licha ya juhudu kubwa za kuufuata mpira huo.

Nusura Yanga iandike bao la pili dakika ya 34 wakati Aziz Ki alipoondoka na mpira bila kubughudhiwa, akiwa nje ya eneo la hatari aliachia kombora kali la mguu wa kushoto, lakini kipa Iddrisu aliruka juu na kuupiga ngumi na kuiokoa Azam kuzama.

Kipa huyo alifanya kazi nyingine kubwa dakika mbili baadaye pale alipokabiliana ana kwa ana na Mudathir Yahaya na kuukoa mpira ambao wachezaji wa Azam walitegea wakidhani kiungo huyo ameotea.

Azam ilipata bao la pili dakika ya 61 kwa mkwaju wa penalti uliotokana na Bakari Mwamnyeto kumchezea madhambi Sillah ambaye aliwasumbua sana mabeki wa Yanga.

Penalti hiyo iliwekwa ndani ya wavu na Prince Dube ambaye alikuwa anafunga bao lake la nne kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Ni kama Azam ilichokoza nyuki kwani baada ya hapo, Yanga ilicharuka na kupeleka mashambulizi mfululizo langoni kwao na haikushangaza ilipopata bao la kusawazisha dakika ya 61, ikiwa ni dakika saba baadaye kwa mkwaju wa faulo wa Aziz Ki.

Baada ya kutokea adhabu nje kidogo nje ya eneo la hatari, alipiga shuti kali ambalo awali lilidakwa na kipa Iddrisu, lakini ukamponyoka na katika harakati za kuudaka ulimgonga kichwani na kujaa wavuni.

Dakika tatu baada ya bao la pili, Yanga ilipachika la tatu, safari hii Aziz Ki akiupata mpira ndani ya eneo la hatari katikati ya mabeki wa Azam FC.

Alichofanya ni kumuangalia kipa amekaa vipi, kwa mguu wa kushoto tena aliupeleka mpira kulia kwa kipa Iddrisu ukatinga nyavuni na kuzusha hoi hoi, nderemo kwa mashabiki wa Yanga.

# SERIKALI YAITAKA MICHEZO YA KUBASHIRI KUPANUA WIGO ZAIDI

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Sanaa Utamaduni na Michezo, Gerson Msigwa, amezitaka kampuni za kubashiri nchini ambazo zinatoa ufadhili kwenye mchezo wa soka pekee kupanua wigo wa ufadhili wao zaidi, hatua itakayoboresha mazingira ya ajira kwa vijana.

Msigwa ameyasema hayo hivi karibuni kwenye Bonanza la kusherehekea miaka 20 tangu kuanzishwa kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini (GBT), ambalo lilifanyika kwenye viwanja vya Green vilivyopo Oysterbay, Dar es Salaam.

Alisema vijana wengi wamejikita kwenye michezo ya aina mbalimbali na kwa kuwapo kwa ufadhili wa kampuni za kubashiri kwenye michezo hiyo kunawaongezea chachu ya ushiriki.

**Katibu huyo alisema michezo ya kubashiri ni mizuri hasa kama kampuni zikisajiliwa na kuzingatia masharti yaliyowekwa na GBT, na kwa kuwa kampuni hizo zinachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi.**

"Kampuni za kubashiri hapa nchini zinazofadhili michezo mbalimbali ikiwamo ya soka zimesaidia kwa kiasi kikubwa kutengeneza mazingira bora ya ajira kwa vijana. Nawapongeza GBT kwa kutimiza miaka 20 kwenye usimamizi wa michezo ya kubahatisha hapa nchini.

"Endeleeni kusimamia vema kazi hii hasa mkiendelea kuzishauri kampuni za kubashiri kuendelea kurudisha faida yake kwa jamii ya Watanzania," alisema.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa GBT, James Mbalwe, alimhakikishia Msigwa kuwa ofisi yake imejipanga kuhakikisha kuwa michezo ya kubashiri inaendelea kuwa na mchango katika sekta mbalimbali hapa nchini hususan kwenye michezo.

Alisema GBT inatekeleza kikamilifu mikakati yake inayolenga kuhakikisha kuwa michezo ya kubashiri inachangia pato la taifa huku akitolea mfano kuwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 michezo hiyo imechangia Sh. bilioni 174.4 katika pato la taifa kwa kwa njia mbalimbali zikiwamo ada za leseni.

"Kwa sasa zipo kampuni nyingi za michezo ya kubahatisha, hata makusanyo yetu yanazidi kupanda tofauti na ilivyokuwa mwaka 2006/2007 ambapo kampuni zilikuwa chache na kujikuta tunakusanya shilingi bilioni mbili tu, ila kwenye miaka ya hivi karibuni makusanyo yanapanda na hakika michango itakuwa mingi zaidi," alisema Mbalwe.

TUPO FITI...



Viungo washambuliaji wa Simba, Clatous Chama (kushoto) na Saido Mtibazonkiza, wakifanya mazoezi ya viungo gym baada ya kutua jijini Cairo, Misri juzi, tayari kwa mchezo wao wa marudiano wa African Football League (AFL), dhidi ya Al Ahly utakaopigwa leo nchini humo. **PICHA: SIMBA**

## Robertinho aanika mbinu

INATOKA UKURASA 24

ni sasa na wapo tayari kwa dakika 90 za kupambana na kupata matokeo chanya.

Kocha huyo alisema anaimani kubwa ya kufanya vizuri katika mchezo huo kwa sababu mechi hiyo itakuwa ya kimbinu na kiufundi kwa kuwa kila mtu anahitaji kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Kuhusu hali ya hewa, alisema haitaweza kuathiri mikakati yao kwa sababu haina tofauti na Dar es Salaam.

Kwa upande wa kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, WIly Essomba Onana, alisema: "Tupo tayari kwa mchezo wa kesho (leo), haitakuwa rahisi ila tumejipanga kuhakikisha tunawapa furaha mashabiki wetu."

Timu hizo zinakutana zikiwa na kumbukumbu ya mechi ya mkondo wa kwanza Ijumaa iliyopita kutoshana nguvu kwa sare ya mabao 2-2, ambayo ni sare ya kwanza tangu timu hizo zilipoanza kukutana katika michuano mbalimbali ya kimataifa.

Timu hizo kila moja imekuwa na rekodi nzuri ya kushinda nyumbani kwake na katika mechi za hivi karibuni kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, mwaka 2019 Simba ilikubali kichapo cha mabao 5-0 nchini Misri kabla ya mchezo wa marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa kushinda 1-0.

Mwaka 2021 kwenye michuano hiyo tena hatua ya makundi, Simba ilishinda bao 1-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa na Al Ahly mechi ya marudiano nchini Misri nayo ikapata ushindi kama huo.

# Mashujaa morali juu wakiifuata Coastal

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Mashujaa FC kimeondoka jana asubuhi jijini Dar es Salaam kuelekea Tanga kuifuata timu ya Coastal Union huku kikiwa na matumaini kibao ya kuibuka na ushindi kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara hapo kesho.

Akizungumza na gazeti hili jana, kabla ya kuanza safari, Kocha wa timu hiyo, Hussein Bunu, alisema kambi ya muda mrefu waliyoiweka jijini Dar es Salaam pamoja na michezo ya kirafiki waliyocheza imeimarisha wachezaji wake kwa asilimia 90.

"Ninashukuru wachezaji wangu wote wapo vizuri kuelekea kwenye mchezo huo, mapungufu yaliyokuwapo nimeyafanyia kazi ili yasijirudie katika mchezo huo," alisema Bunu.

Kocha huyo alisema anaupa umuhimu mkubwa mchezo huo kwani anaamini utakuwa na upinzani mkubwa.

Alisema kila mchezaji ana morali ya juu kuelekea kwenye mtanange huo na kudai lengo lao ni kupata pointi tatu.

"Mpaka sasa sina mchezaji yeyote ambaye ni majeruhi, mikakati yetu ni kushika nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu," alisema.

Mashujaa FC ipo nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kushuka dimbani mara tano na kushinda michezo miwili, sare mbili na kupoteza moja wakati wenyeji wao wa mchezo wa kesho, Coastal Union katika michezo sita iliyocheza haijashinda hata mmoja huku ikipoteza mitatu na kupata sare tatu.

# Michezo

Jumanne Oktoba 24, 2023
Nipashe



Barca yaandaa mechi kumuaga Messi UKURASA 22

HAT-TRICK...



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki (aliyepiga magoti), akishangilia kwa ishara ya kumshukuru Mungu baada ya kuifungia timu yake moja kati ya mabao matatu aliyofunga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC iliyopigwa jana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na timu yake kushinda 3-2. Kulia ni Clement Mzize na Maxi Mpia Nzengeli. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga, Aziz Ki kileleni

## ●●● Wawashusha Simba na Baleke katika mbio za ubingwa na kiatu, hata hivyo...

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Kimataifa wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, jana alifunga mabao matatu 'hat-trick' na kuipa ushindi timu yake ya Yanga wa mabao 3-2 dhidi ya Azam FC na kuirudisha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara huku naye kitawala kilele cha orodha ya wafungaji.

Yanga inakaa juu ya msimamo ikifikisha pointi 15 kama Simba, lakini ina mabao 18, huku Wekundu wa Msimbazi waliokuwa vinara wa ligi hiyo kabla ya mchezo huo wa jana wakiwa na mabao 14.

'Hat-trick' hiyo kwenye mechi ya raundi ya sita ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana Uwanja wa Benjamin Mkapa, inamfanya Aziz Ki kukaa kileleni mwa msimamo wa orodha ya wafungaji akiwa na mabao sita, moja mbele ya Jean Baleke wa Simba aliyekuwa akiongoza na kwa mabao matano.

Katika mabao hayo sita, manne ameyafunga kwa mguu wa kushoto, mawili mguu wa kulia, huku kati ya hayo mawili akiyafungwa kwa faulo na manne mpira ukiwa mchezoni.

**Mabao yote ya jana aliyafungwa kwa mguu wa kushoto, mawili ndani ya boksi na moja nje ya boksi.**

Iliwachukua Yanga dakika nne tu kufika kwenye lango la Azam na kufanya shambulizi la hatari pale Pacome Zouzoua alipuuchukua mpira katikati ya uwanja na kuwahadaa wachezaji wa timu pinzani kabla ya kummegea pande safi, Maxi Nzengeli, akiwa kwenye msitu wa watu, alijikunja na kuachia shuti ambalo lilimpita kipa Iddrisu Abdulai, lakini ukatoka nje kidogo.

Dakika nne baadaye Yanga iliandika bao la kwanza lililowekwa ndani ya wavu na kiungo raia wa Burkina Faso, Stephene Aziz Ki.

Ilikuwa kama masihara, baada ya kuupata mpira kwenye wingi ya kushoto, alipiga chenga moja iliyowapoteza

INAENDELEA UKURASA 23

# Robertinho aanika mbinu za kuipasua Al Ahly Misri

**Na Saada Akida**

LICHA ya kukiri mechi ya marudiano robo fainali ya African Football League dhidi ya Al Ahly nchini Misri itakuwa ngumu leo, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, ametoa siri ya kuweza kushinda ugenini huku akijivunia kikosi alicho nacho kwa kuwa anaweza kumtumia mchezaji yeyote kwa wakati wowote na kupata matokeo.

Akizungumza kutoka nchini Misri jana, Robertinho alisema wachezaji wake wako tayari kwa mechi hiyo na wanaiheshimu Al Ahly kwa kuwa ni timu kubwa na ina uzoefu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini Simba pia ni kubwa na ipo tayari kwa mchezo huo.

Robertinho alisema tayari amewaelekeza wachezaji wake kucheza kama walivyocheza kipindi cha pili kwenye mchezo wa kwanza katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 na kwamba wakifanya hivyo mwanzo mwisho wanaweza kupata matokeo chanya.

Kocha huyo raia wa Brazil, alisema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na wamekwenda Misri kwa lengo la kuhakikisha wanashinda na kutinga nusu fainali.

"Siku zote mimi ni mtu chanya, itakuwa ni mechi ngumu dhidi ya Al Ahly kesho (leo), lakini tumejipanga na kila kitu kinaenda vizuri, nawaamini wachezaji wangu, tupo tayari kushinda.

"Napenda kucheza vizuri na kupata matokeo, tunaingia na mpango tofauti na mechi yetu tuliyocheza awali, sina presha na mchezo wa kesho (leo), licha ya kwamba ni mkubwa, hata mimi nikiwa mchezaji kule Brazil nimewahi kukutana na mechi kama hizi kwenye Uwanja wa Maracana," alisema Robertinho.

Aliongeza kuwa pamoja na ubora na uzoefu walionao Al Ahly barani Afrika, lakini mpira

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >